




**ACT** wataka kamati huru ya uteuzi viongozi Tume Uchaguzi

UKURASA 3




**POGBA KUTUA MAN CITY**

UKURASA 21


# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 8, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580939

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





# Watumiaji wa dawa za kuzuia hedhi hatarini

• **Wataalamu** wa afya watoa angalizo... *Endelea ukurasa 4*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na makandarasi wanaojenga meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu alipokagua maendeleo ya ujenzi wa meli hiyo kwenye Bandari ya Mwanza South, jijini Mwanza jana. Wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi. **PICHA: OWM**

## Ziara ya Majaliwa Mwanza yabaini madudu, acharuka

UKURASA 4

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**POLISI WAWANASA 30 TUHUMA 'PANYA ROAD'**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam katika oparesheni yake ya siku 10...

UKURASA WA 2

**LUGHA YA KUFUNDISHIA YAWAGAWA WABUNGE**

WABUNGE wametoa maoni yao kuhusu maboresho ya sera na mitaala ya elimu...

UKURASA WA 3

**CWT YAGEUKIA KILIO NYUMBA ZA WALIMU**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimetaja mambo sita yaliyotekelezwa kwa...


## Rais Mwinyi asema Royal Tour ni fursa ya kuitangaza sekta utalii

UKURASA 2

MICHEZO NI SIMBA SC VS RUVU LEO UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Mwinyi: Royal Tour ni fursa kuitangaza nchi

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Tanzania imejaliwa kuwa na fursa nyingi za utalii ikiwamo mbuga za wanyama na miji ya urithi, hivyo filamu ya Royal Tour ni fursa ya safari ya kuelekea kuitangaza nchi.

Akizungumza katika uzinduzi wa filamu hiyo visiwani Zanzibar katika Hoteli ya Golden Tulip Unguja, Rais Mwinyi alisema filamu hiyo imelenga kuitangaza Tanzania katika utalii, uwekezaji na utamaduni.

Dk. Mwinyi alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa wazo la kutayarisha filamu hiyo kwa ajili ya kutangaza nje ya nchi fursa na vivutio vilivyopo nchini.

Alisema Rais Samia amejitoa na kushiriki kikamilifu katika filamu hiyo kwa kujituma kiasi cha kuwa mshiriki nambari moja katika filamu. "Nachukuwa nafasi hii kwa dhati kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa mshiriki aliyeongoza katika filamu hiyo, sawa na kuwa mhusika nambari moja," alisifu.

Dk. Mwinyi aliwataka wadau wa sekta ya utalii Zanzibar, wakiwamo wamiliki wa hoteli na kampuni kujipanga kutoa huduma bora za utalii kwa ajili ya kutangaza utalii kufuatia matokeo ya utalii katika filamu hiyo.

"Nawataka wadau wa sekta ya utalii mjipange vizuri kwa sababu najuwa tutapata mafuriko ya watalii mara baada ya kuzinduliwa kwa filamu hii na kuonekana na watu wanaokaribia bilioni moja duniani kote," aliagiza.

Aliongeza: "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumefanya uamuzi muhimu wa kuvikodisha visiwa vidogo vidogo viweze kutumika kwa ajili ya kutangaza sekta ya utalii duniani kwa wawekezaji kuwekeza."

Mjumbe wa Kamati ya Royal Tour na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitega Uchumi na Uwekezaji (ZIPA), Sharifu Ali Sharifu, aliwapongeza viongozi wakuu Rais Samia pamoja na Rais Mwinyi kwa kujitoa moja kwa moja kushiriki filamu hiyo ambayo imeitangaza nchi.

Alisema uzinduzi wa filamu hiyo ni ushahidi wa kuimarika kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika ushirikiano wa pande mbili za viongozi hao.

Alifahamisha tayari filamu hiyo inatarajiwa kuonyeshwa na jumla ya vituo 350 Marekani ambapo zitawafikia watu milioni mbili wa Marekani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Filamu ya Royal Tour, Dk. Abasi Hassan, alisema filamu hiyo iliyotayarishwa na kuzinduliwa, inavyo vigezo vya ngazi ya Holywood na inakubalika



Shimo likiwa katikati ya barabara ya Samora, Posta jijini Dar es Salaam, huku vyombo vya moto vikipita kwa tahadhari jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lugha ya kufundishia yawagawa wabunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wametoa maoni yao kuhusu maboresho ya sera na mitaala ya elimu nchini huku mvutano ukibuka kwenye matumizi ya lugha ya kufundishia na kushauri ufanyike utafiti ili kupata mwafaka.

Akitoa maoni jana kwenye mkutano ulioandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo, alishauri nchi iwe na msimamo kwenye mabadiliko hayo huku akitaka wizara ifanye utafiti kwenye nchi zingine kuhusu matumizi ya lugha kwa kuwa maoni ya wadau hayaleti mwafaka.

"Suala la lugha mmeliona hapa kwa kutafuta maoni halitaisha, kila mmoja anachangia anavyoona yeye, wengine wanasema umuhimu wa Kiingereza, wengine wanasema umuhimu wa Kiswahili, wengine wanalinganisha na China, kuna haja ya kufanya utafiti waliopitia hii michakato kuona wenzetu walifanya nini? Twende kwenye utafiti ili tuje na suluhisho la mwisho," alisema.

**WALICHOSEMA WABUNGE**

Mbunge wa Singida Mjini (CCM), Mussa Sima, alisema Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 haisemi lugha ya kufundishia ni ipi na kushauri utafiti ufanyike.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Shally Raymond, alisema kuna wimbi la watu wanasema kitumike Kiswahili na kwamba wanataka Tanzania ijifungie.

"Tunataka kujifungia Tanzania kwa sababu Kiswahili Tanzania ni lugha yetu mama na watoto wetu wanatumia kwa kuwa ni lugha namba moja, sasa kuungana tunaungana na nini? Hivi kama Baiolojia unaiingizaje kwenye Kiswahili, bado Kiingereza kinapaswa kupewa kipaumbele, tena kianzie darasa la kwanza," alisema.

Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi, alisema Tanzania isipotumia Kiingereza, Watanzania watapata tabu kupata ajira nje ya nchi na kushauri lugha ya Kiingereza ipewe kipaumbele.

Mbunge wa Singida Kaskazini (CCM), Ramadhan Ighondo, alisema utafiti aliofanya amebaini watoto wanapotoka shule ya msingi, wanatoka wakiwa na uelewa lakini wakifika sekondari wanakunja sura kutokana na lugha.

Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema badala ya kulikimbia tatizo ni vyema kulitibu kwa kuwa kama hakuna walimu wa Kiingereza, wafundishwe na kupatikana walimu stahiki wa kufundisha lugha hiyo.

Awali, Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, alisema kazi ya mitaala itakamilika vizuri wakati ambapo rasimu ya maboresho ya sera itakapokuwa imekamilika ili visiongee tofauti na ifikapo mwishoni mwa mwezi Desemba mwaka huu kuwe na rasimu ya maboresho ya sera na mitaala yake na mwezi Januari mwakani (2023) uanze mchakato wa kuomba idhini serikalini.

Alisema dunia hivi sasa ina msukumo mkubwa wa mageuzi ya elimu ambapo kuna mpango wa kusamehe madeni au kupata misaada kwenye nchi zinazofanya mageuzi ya elimu.

"Mageuzi tunayokwenda nayo yatakuwa ni makubwa kwa nchi yetu, hatutaki kubahatisha, hatuhitaji kukurupuka, ndiyo maana tunahitaji sana kusikiliza maoni yetu," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
02.05.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **04.05.2022 hadi 17.05.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi,** gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW052Z / ZG3212**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita 28.4** |
| **Upana** | - | **Mita 5.0** |
| **Kimo** | - | **Mita 5.6** |

3. Njia itakayotumika: **Holili hadi Moshi kupitia Soweto,** gari litasafiri muda wa mchana tu **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

216843002

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


# Polisi wawanasa 30 tuhuma 'panya road'

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam katika operesheni yake ya siku 10 ya kuwasaka vijana wanaofanya uhalifu mitaani usiku, maarufu panya road, limewatia mbaroni watuhumiwa 31 wanaodaiwa kujihusisha na unyang'anyi, kujeruhi na kuiba.

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa operesheni hiyo ilianza Aprili 27, mwaka huu hadi juzi na itakuwa endelevu.

Alisema katika operesheni hiyo wamewakamata watoto wenye umri kati ya miaka 13 na 20 ambao huvunja nyumba, kujeruhi na kuiba vitu mbalimbali.

"Watuhumiwa wakati wanafanya uhalifu hutumia mapanga, visu, nondo na mikasi mikubwa. Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na raia wema kupokea taarifa mbalimbali za wahalifu na linaahidi kuzifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwakamata kabla ya kutenda uhalifu," alisema.

Kamanda Muliro alisema kuwa katika mahojiano ya kina, Jeshi la Polisi limebaini watuhumiwa hao wamehusika kwenye vitendo hivyo na kuonyesha baadhi ya vitu walivyoiba zikiwamo luninga 12 na simu nne za kiganjani.

"Jeshi la Polisi linatoa onyo na halitasita kuwakamata ambao wamekuwa wakipokea mali za wizi zinazotokana na matukio ya kihalifu," alionya.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muliro alisema wanamshikilia Fakhi Hamisi (30), mkazi wa Unio na wenzake 33 wakidaiwa kukutwa na dawa za kulevya aina ya bangi magunia 10 yenye uzito wa kilogramu 180, kete 497 na puli 48.

Alisema watuhumiwa hao wamekamatwa maeneo ya Kinondoni baada ya kupokea taarifa za kihalifu na wamekutwa na sare moja ya Jeshi la Wananchi (JWTZ), darubini, kisu, blanketi na viatu vya jeshi, pikipiki sita na bajaji moja.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (kulia) akizungumza na wafanyabiashara wa Soko la Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani ambayo inafikia kilele chake Mei 15 mwaka huu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# ACT wataka kamati huru uteuzi viongozi wa NEC

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema mchakato wa kupata Katiba Mpya unapaswa kuanza sasa badala ya mwaka 2025 huku kikipendekeza kuwapo kamati huru ya uteuzi wa viongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Katika hotuba yake wakati wa kongamano la pili la Tume Huru ya Uchaguzi kuelekea Katiba Mpya, jijini Mwanza jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Duni Haji, alisema kikosi kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan cha kukusanya na kuchambua maoni ya wadau wa siasa kimetoa ripoti yake ya awali.

Alisema sehemu ambayo hawakubaliani ni maoni kuwa mchakato mzima wa Katiba Mpya uanze baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

"ACT Wazalendo tunasema mchakato wa mabadiliko ya tume ya uchaguzi na Katiba Mpya vianze sasa. Kuhusu katiba, mchakato mgumu zaidi ni kujenga mwafaka wa kitaifa.

"Bila mwafaka wa kitaifa, hakuna Katiba Mpya, tutaendelea kuvutana miaka nenda rudi bila kupata Katiba Mpya," kiongozi huyo alitoa angalizo.

Duni alisema ni lazima mazungumzo ya wadau wa Katiba Mpya yafanyike ili kupata mwafaka wa kitaifa kuhusu namna ya kuuendea mchakato wa Katiba Mpya.

Alisema kwa ujumla wanakubaliana kwenye maeneo mengi ya muda mfupi na wa kati yaliyopendekezwa na kikosi kazi cha Rais Samia.

"Tunakubaliana kuhusu kufunguliwa upesi kwa mikutano ya hadhara, kufanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Vyama vya Siasa na kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi.

"Kwa hili la kuandikwa kwa sheria mpya ya vyama vya siasa, ninapenda kumkumbusha Mheshimiwa Rais kuhusu ahadi yake ya kuandikwa kwa sheria mpya kwenye Bunge hili la Bajeti ili nchi ipate sheria mpya ya vyama vya siasa tunapotimiza miaka 30 ya vyama vingi nchini," alisifu.

**TUME HURU**

Kuhusu Tume Huru ya Uchaguzi, Duni alisema ikiwapo nchini, itahakikisha Katiba Mpya yenye maoni ya wananchi inapatikana.

"Mara zote tumesema tutakuwa tunajidanganya iwapo tutakwenda kwenye kura ya maoni ya Katiba Mpya bila kuwa na tume huru. Tutapoteza tena mabilioni ya Watanzania iwapo tutataka katiba inayopendekezwa ipigiwe kura ya maoni ikisimamiwa na tume hii ya sasa ya uchaguzi," alitahadharisha.

Alisema ili kupata Tume Huru ya Uchaguzi, ACT Wazalendo wanapendekeza kuandikwa upya kwa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi.

Duni alidai kuwa sheria ya sasa inaifanya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Tunataka tume itakayoweza kusimamia kura ya maoni ya Katiba Mpya na uchaguzi ujao kwa haki na kujiamini. Tumependekeza kuundwa kwa kamati huru ya uteuzi wa viongozi wa tume ambayo itajumuisha Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Mwenyekiti na Jaji Mkuu wa Zanzibar kama Makamu Mwenyekiti," alisema.

Duni alisema ACT-Wazalendo inapendekeza wajumbe wa kamati hiyo wawe: Rais wa Tanganyika Law Society (TLS), Zanzibar Law Society (ZLS), mtu mmoja atakayeteuliwa na mkuu wa shughuli za serikali bungeni na mwingine atakayeteuliwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Pia chama hicho kimependekeza endapo hakuna kambi rasmi ya upinzani bungeni, basi mtu huyo atolewe katika chombo kinachojumuisha vyama vyenye wabunge bungeni.

"Mtu mmoja kutoka asasi ya kitaifa ya masuala ya sheria na haki za binadamu Tanzania Bara na mwingine kutoka kwenye asasi kama hiyo Tanzania Zanzibar," alipendekeza.

Duni aliendelea: "Kwa vyovyote vile, angalau theluthi ya wajumbe wa kamati lazima wawe wanawake. Mbali na hilo, tunataka kuwe na sifa maalum za wajumbe wa tume zitakazowaongoza ili kuhakikisha wanaoteuliwa wanakuwa watu wenye weledi na wasiogemea upande wowote."

Alikumbusha yaliyotokea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu mwaka 2020 na kueleza kuwa ACT-Wazalendo inapambana kuhakikisha uchaguzi ujao unafanyika kwenye mazingira ya uhuru, haki na usawa.

Alisema bila Tume Huru ya Uchaguzi, Watanzania wataendelea kukata tamaa na itakuwa vigumu kuwashawishi kupiga kura.

# CWT yageukia kilio nyumba za walimu

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimetaja mambo sita yaliyotekelezwa kwa walimu chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan huku kikiomba mkazo zaidi kwenye ujenzi wa nyumba za walimu husussan maeneo ya vijijini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kaimu Rais wa CWT, Dinnah Mathamani, alisema uhaba wa nyumba za walimu ni tatizo kubwa hasa vijijini.

"Walimu wanaoajiriwa wengi watakwenda vijijini ambako kuna uhaba wa walimu, zaidi kuliko mijini, lakini kule wanakokwenda nyumba za kupanga hakuna, watu wanaishi tu kijamaa, kuna nyumba ya mwenyekiti au mratibu.

"Kuna wakati walimu wetu wanapokewa kwenye jamii ile wanaishi katika familia kadhaa bila kuwapo na nyumba ambayo walimu wanaweza kuishi kwa amani na kuandaa masomo, lakini mtu anahitaji kuwa na 'privacy' (faragha) yake," alisema.

Alieleza kuwa serikali katika bajeti yake ya 2022/23 imetenga Sh. bilioni 55.57 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 809 ambazo zitakaliwa na kaya 1,916 za walimu na kuomba bajeti iongezwe kutokana na kuwa na uhaba wa nyumba hizo.

"Kupanga bajeti na kuitamka ni jambo la kwanza lakini utekelezaji ni jambo lingine, sisi Chama cha Walimu tunaomba serikali yetu kwa nia hiyo njema ya kuweka bajeti, kuona umuhimu wa walimu na kuwajengea mazingira mazuri, ikasimamie hilo na hizo fedha zitumike kwa ajili ya kuwajengea walimu nyumba ili kuishi mazingira mazuri na kufundisha wanafunzi vizuri," alisema.

Akizungumzia mambo sita yaliyotekelezwa na Rais, kiongozi huyo alisema serikali imeendelea kutekeleza mambo mbalimbali kulingana na mahitaji ya walimu ikiwamo upandishaji wa madaraja ambapo kwa mwaka 2021/22 walimu 127,000 walipandishwa madaraja huku wengine 52,000 wakitarajia kupandishwa mwaka huu.

Pia alisema serikali imeajiri walimu na hivyo kupunguza uhaba mkubwa wa walimu uliokuwapo ambapo kuna baadhi ya shule walimu walikuwa wakibeba mzigo mkubwa wa vipindi darasani.

"Kuna maeneo vijijini walimu wapo watano au sita na hata wanne na malengo ni yale yale wanafunzi wafaulu kwa kiwango kinachotakiwa, ilikuwa ni wakati mgumu kwa walimu lakini bahati nzuri kilio kimesikika, serikali imekuwa ikiongeza walimu kwa awamu ambapo awamu ya kwanza 13,000, ya pili 7,000, ya tatu 6,000 kwa mwaka 2020/21.

"Walimu walikuwa na mzigo mkubwa, walikuwa wanafundisha vipindi 35 hadi 40, kuongezeka kwa walimu watakwenda kuwapunguzia mzigo wa vipindi kwa walimu na kuwapa fursa ya kujiandaa vizuri kufundisha," alisema.

Kadhalika, alimshukuru Rais kwa kusikia kilio chao cha kuwapatia stahiki zao waliokumbwa na vyeti feki lakini na wale wa darasa la saba waliokuwa wamefika muda wa kustaafu.

Alisema kwa mwaka 2021 pamoja na janga la UVIKO-19, kupanda kwa mafuta, vita vya Ukraine na Russia, Rais aliweka nguvu kazi na ujenzi wa madarasa 15,000.

"Tunalipongeza kwa kufanya hili kwa ajili ya Watanzania na wanafunzi, walimu sasa wanafundisha kwa nafasi sasa, zamani mwalimu alikuwa akifundisha wanafunzi wamejazana hadi karibu na ubao, na sasa hakuna msongamano kwenye madarasa," alisifu.

Kuhusu madeni mbalimbali, Kaimu Rais huyo alisema serikali imeendelea kulipa siku hadi siku kwa madeni yaliyohakikiwa na kuomba yaliyopo yahakikiwe na yalipwe kwa wakati ili walimu wawe na utulivu shuleni badala kushinda kwenye ofisi za wakurugenzi wa halmashauri kufuatilia madai.

"Walimu tunamshukuru Rais Samia kutokana na kuona kwa muda mrefu mishahara haijapandishwa na amesema jambo letu lipo pale pale, tunasubiri hilo la mishahara kwa hamu kwa kuwa lipo hatua ya mwisho ya utekelezaji," alisema.

Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, alisema kutokana na yanayofanywa na serikali, ni wajibu wao walimu sasa kufundisha ipasavyo.

## HABARI KITAIFA

# Watumiaji wa dawa kuzuia hedhi hatarini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATAALAMU wa afya wametoa angalizo kwa wanawake wanaotumia dawa za kuzuia hedhi pasi na ushauri wa daktari kwamba wako hatarini kupata madhara, yakiwamo maradhi ya moyo.

Katika mazungumzo maalum na Nipashe ofisini kwake mjini hapa jana, Shomari Masenga, Daktari wa Magonjwa ya Kinamama Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe, alitaja dawa hizo kuwa zimegawanyika katika makundi matatu Primolut Tables, Ergometrine Injection na Combined Oral Contraceptive pill.

Akifafanua zaidi matumizi ya dawa hizo, daktari huyo alisema Primolut Tables ni dawa wanazopewa wanawake ambao wanatoka damu nyingi na wamepoteza mpangilio wao wa kuingia hedhi.

"Inatengenezwa na 'component' ya projestine ambayo inafanya kazi ya kupunguza uzito kwenye ukuta wa ndani wa mfuko wa uzazi ambao ukipungua ndiyo damu inatoka nyingi.

"Madhara ya dawa hizi ni kubadilisha mzunguko wa hedhi, kukosa usingizi, kuongezeka uzito, kizunguzungu, kukosa hisia za kufanya mapenzi na kuwa na hasira," alifafanua.

Daktari huyo, akizungumzia matumizi ya Ergometrine Injection, alisema ni dawa zinazotumiwa na mama mjamzito baada ya kutoka kwa kondo la nyuma na kupoteza damu nyingi na zinatengenezwa kwa 'component' ya Ergometrine Maleate.

Hata hivyo, daktari huyo alitoa angalizo kuwa dawa hizo sasa hazitumiki hospitalini kutokana na madhara yaliyobainika.

"Husababisha 'heart attack' (shambulio la moyo) kwa mtumiaji, moyo unaweza ukafa kwa sababu ya kukosa damu, seli za moyo zitashindwa kufanya kazi, kifua kujaa maji hadi kupelekea kifo. Madhara mengine ni kupumua kwa shida," alisema.

Kuhusu Combined Oral Contraceptive Pill, daktari huyo alisema aina hiyo ya dawa ni kwa ajili ya uzazi wa mpango, akifafanua: "Hii inatumika kuchelewesha siku na kutibu kama unavuja damu nyingi. Dawa hizi zinafanya kazi ya kuzuia kutoka kwa damu ya hedhi, mara nyingi dawa hizi wanapewa ambao wanatoka damu kupitiliza pamoja na wanaotaka kuchelewesha hedhi.

"Zimetengenezwa kwa component aina mbili -- Oestrogen na Progestine. Zinafanya kazi gani? Zinazuia upevushaji wa yai, kusababisha ute wa shingo ya kizazi kuwa mzito na mbegu za kiume kushindwa kupita.

"Madhara yake kiafya ni kwamba zinasababisha kutoka damu kidogo kidogo, shida ya moyo, damu kuganda kwa wenye umri kuanzia miaka 35.

"Madhara mengine ya dawa hizi zote ni makubwa kwa sababu yanasimamisha ufanyaji kazi wa vichocheo katika mwili, wengi wanaotumia dawa hizo ni wale ambao wanakuwa na 'matukio'.

"Mtu anakua anataka kwenda kwa mpenzi wake au kwenda sehemu yoyote hataki kuwa kwenye hedhi, basi anakunywa dawa hizi ili kuzuia," Dk. Masenga anafafanua.



Wasamaria wema wakijaribu kulinasua gari iliyokwama katika barabara ya Nike kuingia Goba Tegeta A, mkoani Dar es Salaam baada ya kuharibika kwa mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ziara ya Majaliwa Mwanza yafichua 'madudu', acharuka

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa ameagiza kushikiliwa kwa pasi za kusafiria za wataalamu wa kampuni ya GAS Entec ya Korea Kusini wanaojenga meli ya MV Hapa Kazi Tu jijini Mwanza hadi wakamilishe kazi yao.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana alipozungumza na wananchi na viongozi wa mkoa huo mara baada ya kukagua ujenzi wa meli hiyo katika eneo la Mwanza South wilayani Nyamagana.

"Nimemwagiza Ofisa Uhamiaji wa Mkoa akamate pasi zao mara moja na ahakikishe hakuna mtu anatoka nje ya mkoa huu hadi hii kazi ikamilike. Nimeambiwa wako saba, lakini hapa wako watatu. Watafuteni hao wengine wako wapi?" alihoji.

Wenye pasi hizo ni Mkurugenzi wa GAS Entek, Dong Myung Kwak na wasaidizi wake, Kyunghan Choi na Kyuh Yun Kwak ambaye ni mtoto wa mkurugenzi huyo.

"Nimeingia ndani kukagua kazi ya ujenzi lakini sijaridhika nayo. Katika maelezo yao nimebaini kuwa kampuni tuliyoingia nayo mkataba ya GAS Entec imeuza 'share' (hisa) zake bila serikali kuarifiwa. Waliouziwa walipokuja walishangaa kuona ujenzi wa meli kwa sababu suala la ujenzi liko nje ya mauziano yao," alibainisha.

Waziri Mkuu aliyekuwa mkoani Mwanza kwa ziara ya siku moja, alisema serikali imeshalipa asilimia 80 ya gharama za ujenzi wa meli hiyo lakini kazi iliyofanyika kwa mujibu wa mkataba ni asilimia 65 tu. Alisema taarifa alizonazo zinaonyesha kuwa wafanyakazi walikuwa 118 lakini sasa wamebakia 22 tu.

"Haiwezekani tuwalipe hela hiyo, kazi haiendi kama ilivyopaswa. Tena wamepunguza wafanyakazi kutoka 118 hadi 22, tunajuaje kama kesho watawaondoa hao 22 na wao wenyewe wapande ndege kurudi kwao au waende Nairobi kupanda ndege?" Majaliwa alihoji.

Alisema ameshawasiliana na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameridhia hatua hiyo, akionya: "Hawa watu wasiondoke hadi kazi ikamilike na kama wataondoka, basi atakayewadhamini ni balozi wao. Serikali tutaendelea kuwasiliana na Balozi wa Korea Kusini na tunaamini kazi hii itakamilika. Wizara husika simamieni na kuhakikisha kazi inakamilika kwa mujibu wa mkataba."

Mkurugenzi wa GAS Entek, Kwak alimweleza Waziri Mkuu kuwa amelazimika kupunguza wafanyakazi kwa sababu ana makontena matatu bandarini ambayo anatarajia yataanza kutoka baada ya wiki mbili.

Kauli ya Kwak ilikanushwa na Meneja Mradi ambaye pia ni Mhandisi Mkazi, Lt. Col. Vitus Mapunda kwamba makontena matatu ni sehemu ndogo sana ya kazi iliyobakia na ambayo inatakiwa kuwa imefikiwa.

Gharama za ujenzi wa meli hiyo ni dola za Marekani milioni 39 sawa na Sh. bilioni 80.

Baada ya kukagua ujenzi wa meli hiyo, Majaliwa alikwenda eneo la Kigongo Busisi kukagua maendeleo ya ujenzi wa daraja la JPM lenye urefu wa kilomita tatu. Akiwa katika eneo hilo aliiagiza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ikutane na watendaji wa Idara ya Kazi Mkoa wa Mwanza ili kuhakikisha watumishi katika mradi huo wanalipwa stahiki zao ipasavyo.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa Mbunge wa Sengerema, Hamisi Tabasamu aliyedai kuwa licha ya mradi huo kuendelea, watumishi wamepungua na wanakimbilia katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Mhandisi Mshauri wa mradi huo, Benjamin Michael alisema awali kulikuwa na wafanyakazi 813 na sasa wamebaki 744 baada ya wengine kuacha kazi.

Majaliwa pia alishuhudia 'upigaji' wa fedha za serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema baada ya kuambiwa mradi wa jengo la halmashauri hiyo wa Sh. bilioni 2.7 umetelekezwa na makandarasi.

Akitoa salamu za Mkoa wa Mwanza, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel alisema watahakikisha watu wote wanaotafuna fedha za umma wanachukuliwa hatua.

Waziri Mkuu alilazimika kutaja hadharani majina watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema waliotafuna fedha za halmashauri hiyo.

Majaliwa aliwasoma watumishi hao na kuwataka wasimame ili wenzao wawaone huku akitoa miezi miwili warudishe fedha hizo.

Alimwagiza mweka hazina kuwaandikia barua rasmi kwa kila mmoja Ili warudishe fedha hizo na kusisitiza kuwa mtu yeyote anayedhani awamu hii ni ya mchezo, afute mawazo hayo.

Alikabidhi kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ajili ya hatua zaidi.

## Wamiliki maduka ya dawa muhimu waiangukia serikali

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wamiliki wa Maduka ya Dawa Muhimu za Binadamu wameiomba serikali isikilize kilio chao cha kupewa kibali cha kufanya shughuli hiyo mijini.

Mwenyekiti taifa wa chama hicho, Juma Mganga, aliwasilisha kilio chao hicho juzi mkoani Dar es Salaam alipozungumzia kadhia ya kufungiwa maduka yao na kusambaa kwa video fupi ikimwonyesha mhudumu kwenye duka akishindwa kujua aina za dawa.

Mganga ambaye pia ni Mwenyekiti wa Wamiliki wa Maduka ya Dawa Muhimu Mkoa wa Dar es Salaam, alisema ombi lao kwa serikali ni kuwawezesha kupewa vibali vya kuendelea kufanya shughuli hiyo mjini.

Kuhusu video fupi iliyosambaa mtandaoni ikionyesha mhudumu kwenye duka la dawa akishindwa kujua aina ya dawa, kiongozi huyo alidai siyo mwanachama wao.

"Tunawajua walioziten-geneza kwa sababu na sisi tunaishi na jamii, muundo wetu wa chama unauona pale, tunapata taarifa ambayo ni ya chini kwenye chanzo, watu kwenye zile video fupi siyo wanachama wetu," alisema.

Mganga alisema ujio wa maduka hayo ulilenga kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kusaidia upungufu na ukosefu wa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma.

Alidai kuwa kwa sasa wamefika mahali mamlaka zinazosimamia maduka ya dawa nazo zimeingia kwenye biashara.

Alisema chama chao kitaifa kina vyama 22 ambavyo vipo hai vinavyosimamia maduka ya dawa kwenye mikoa na wilaya tofauti.

"Vyama vyote vimepata hili sekeseke la kufungiwa Aprili 27, mwaka huu tulikuwa na kikao cha pamoja cha taifa Dodoma, tumegundua tatizo hili ni kubwa, wanavyopewa zile taarifa kupitia video fupi inayosambaa mtandaoni siyo za kweli.

"Tunaomba watumie vyombo vyao vikafanye kazi, kama hii mamlaka wenyewe ni wafanyabiashara wao wanasimamiwa na nani? Tunataka mamlaka zilizo juu na zenyewe zione hili wajue wapo Mungu watu wametokea kwenye tasnia hii," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Mwadini, alisema hawapo kama walivyotafsiriwa kupitia video hiyo.



Baadhi ya wafanyakazi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), wakifanya usafi katika Mtaa wa Simu uliopo Posta jijini Dar es Salaam jana na kutoa vifaa vya kufanyia usafi kwa Serikali ya Mtaa huo katika kuunga juhudi za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kutunza mazingira. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri awapa msaada wa fedha wanafunzi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameadhimisha miaka 60 ya kuzaliwa kwake kwa kuchangisha Sh. milioni 41.616 za kugharamia masomo kwa wanafunzi wenye uhitaji.

Pia ameitaka jamii kuangalia namna ya kuwasaidia wanafunzi wenye uwezo wa kimasomo lakini wameshindwa kuendelea na masomo kutokana na vikwazo mbalimbali vikiwamo vya kifedha.

Maadhimisho hayo yalifanyika juzi mkoani Dodoma kwa waziri huyo kushiriki Misa Takatifu kwenye Kanisa la Parokia ya Kiwanja cha Ndege na kufuatiwa na chakula kwenye Hoteli ya St Gasper.

"Tukiwa na utaratibu wa kusaidia, basi tutakuwa tumewasaidia wanafunzi wengi wenye uwezo wa kimasomo lakini wameshindwa kuendelea na masomo kutokana na changamoto za kifedha," alisema. Dk. Mabula alisema lengo la kuitumia siku yake ya kutimiza miaka 60 ya kuzaliwa kwake kuchangisha fedha ni kutaka kuwanufaisha wanafunzi wenye taaluma mbalimbali na kutaka kila mtu kutoa michango kulingana na alivyoguswa.

Askofu wa Jimbo Katoliki Mtwara, Titus Mdoe, alimpongeza Dk. Mabula kwa uamuzi wake wa kutoa shukrani kwa Mungu kwa zawadi ya uhai aliyoipata kufikisha miaka 60 sambamba na uamuzi wa kuchangisha fedha za kusaidia masomo, jambo alilolieleza kuwa ni uamuzi wa busara.

"Mama ana jambo lake, naye ni mpenzi wa maskini wa roho na mali ndiyo maana umechagua kuwasaidia maskini, vijana wanaokosa pesa za ada lakini umeamua kushiriki kutafuta pesa za kuwasaidia," alipongeza Askofu Mdoe. Kiongozi huyo alibainisha kuwa wapo vijana wengi walioko vijijini wanashindwa kuendelea na masomo kutokana na hali ya wazazi wao, jambo lililomsukuma Waziri Mabula kuja na wazo la kuchangisha fedha wakati wa misa ya kusheherekea kutimiza miaka 60 ya kuzaliwa.

Baadhi ya wanafunzi walionufaika walisema mfuko huo umekuwa ukitoa fursa za kimasomo kwa wale wanafunzi wanaotoka familia zenye kipato duni.

Thomas Kichenje anayesoma Stashada ya Utawala wa Biashara Chuo cha STeMMUCo Mtwara, alisema bila ya ufadhili wa mfuko wa kichungaji, asingekuwa chuoni huko kwa kuwa baada ya kuomba vyuo kadhaa, alikosa ufadhili.

Mwanafunzi mwingine Frank Kiwanga anayesomea masomo ya sheria SAUT Mtwara, alisema alikosa mkopo wa elimu ya juu mara nne lakini kupitia msaada wa mfuko wa kichungaji ameweza kusoma shahada hiyo.

Maadhimisho ya kutimiza miaka 60 ya kuzaliwa Dk. Mabula kwa kuchangisha fedha yamefanyika pia katika mikoa ya Mbeya, Mwanza na Mtwara. Uchangiaji wa mfuko huo unafanyika kwa wananchi kununua kadi za kuchangia, udhamini wa wanafunzi na mchango wa hisani kupitia chakula ambapo fedha zinazochangwa hutumika kulipia gharama za bweni, ada, bima pamoja na mafunzo ya vitendo.

# Madiwani waingiwa hofu mfumo malipo kahawa

**Na Lilian Lugakingira,** KYERWA

BAADHI ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera wameiomba serikali kuungalia upya mfumo wa kuwalipa wakulima wa kahawa kupitia akaunti za benki ili usiwaumize kwa kuwacheleweshea malipo yao.

Wakizungumza juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani baada ya meneja masoko wa chama kikuu cha ushirika katika wilaya za Karagwe na Kyerwa (KDCU) kuwasilisha taarifa ya utaratibu mpya utakaotumika kuwalipa wakulima wa kahawa, madiwani hao walisema mfumo uliopangwa hauwezi kukamilika ndani ya saa 24 kama inavyoelezwa.

Diwani wa Bugara, Frednand Bishanga, alisema mfumo wa kumlipa mkulima umewekewa mzunguko ambao malipo hayawezi kumfikia mhusika ndani ya saa 24 baada ya mnunuzi kulipa kupitia akaunti ya Bodi ya Kahawa nchini (TCB).

"Tumeelezwa hapa mnunuzi baada ya kukamilisha taratibu zote za manunuzi atalipa fedha kupitia akaunti ya TCB, baada ya hapo TCB iweke fedha katika akaunti za Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS), na vyama hivyo viwalipe wakulima kwa kuweka fedha katika akaunti zao, tuwe wa kweli hapa kuna tatizo, huu mchakato hauwezi kukamilika ndani ya muda wa saa 24," alisema. Bishanga alisem hofu yake ni visingizio vitakavyojitokeza ikiwamo kuambiwa kuna tatizo la mtandao na kuiomba serikali kutafuta namna bora ambayo mkulima atapata fedha yake kwa haraka.

Diwani wa Viti Maalumu, Devotha Byashara, alisema utaratibu wa kulazimisha mkulima fedha zake zilipwe kupitia akaunti za benki linapaswa kuangaliwa kwa umakini kwa sababu wapo wazee ambao hawana nguvu za kwenda huko kufuata malipo.

Alisema miaka ya nyuma KDCU waliwahi kutumia mfumo huo wa benki na katika simu zao, lakini ulizua malalamiko ya baadhi yao kutopata yanayostahili.

Akiwasilisha taarifa yake katika kikao hicho, Meneja Masoko wa KDCU, Stephen Sililo, alisema kuwa baada ya mnada wanunuzi watapaswa kulipa fedha hizo TCB na bodi hiyo itaziweka kwenye akaunti za AMCOS ndani ya saa 24 ili kuhakikisha usalama wake.

"Tulikaa na kuazimia kuwa turudi katika mfumo wa kuwalipa wakulima wa kahawa kupitia akaunti za benki za wanachama, hii ni kutokana na uzoefu na matatizo tuliyoyapitia, likiwamo la baadhi ya viongozi katika vyama vya ushirika kutokuwa waaminifu na kusababisha wakulima kutopata haki yao ipasavyo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Rashid Mwaimu alisema kahawa ya mkulima itauzwa kupitia ushirika na masoko yote yatafanyika kwa mnada na wanunuzi wanaruhusiwa kulinunua AMCOS.

"Lengo ni kuongeza ushindani na kuzisimamia kwa umakini mkubwa sera zote zinazolenga kumnufaisha mkulima, ili kuhakikisha kipato chake kinaongezeka kupitia hayo masoko ya kahawa, mwongozo utatoka wakati wowote kuanzia sasa, hivyo wadau mjiandae," alisema Mwaimu. Makulima Yustinian Eustace ambaye ni mkazi wa Kitongoji cha Ibwera wilayani humo, aliuelezea utaratibu huo kuwa ni mzuri kwa sababu benki haiwezi kumdhulumu mkulima haki yake.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waliohusika na madudu MSD wachukuliwe hatua

**WIKI** hii, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alifungua Wiki ya Ununuzi wa Umma jijini Arusha huku akianika madudu yaliyofanywa na baadhi ya taasisi katika ununuzi wa vifaa muhimu, ikiwamo upotevu wa fedha za UVIKO- 19 zilizotolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali na zahanati.

Madudu hayo yaliyoibuliwa na Waziri Mkuu, yamekuja wiki chache baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwasilisha ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2020/21 ambayo ilionyesha matatizo makubwa katika matumizi ya fedha za umma.

Katika madudu hayo, Majaliwa alitolea mfano Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ilivyotumia vibaya fedha za umma katika ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa kuongeza bei ya vitu hovyo tofauti na bei halisi. Watendaji hao katika ununuzi huo, walinunua vifaa mara mbili hadi tano ya bei halisi, hali inayoonyesha bayana kuna upigaji wa kutisha katika baadhi ya taasisi za serikali.

Kipimo cha sukari, mathalan, MSD ilinunua kwa Sh. 300 badala ya Sh. 150 huku kipimo cha mkojo kikinunuliwa kwa Sh. 780 badala ya Sh. 200. Pia walitakiwa kununua kipimo kidogo cha hamolojia ya mwili kinachouzwa Sh. 2,100 lakini wakanunua kwa bei ya zabuni Sh 4,500.

Hiyo ni kidogo lakini kufuru zaidi ni pale walipononunua kipimo cha kuangalia ufanyaji kazi wa figo kwa Sh. 40,000 badala ya sh. 6,000 na seti moja ya vitendanishi kwa ajili ya awamu moja ya kusafisha damu kwa Sh. 189,000 tofauti na Sh. 65,000 ambayo ni bei halisi. Hawakuishia hapo bali walizidi kufanya kufuru kwa kununua mashine ndogo ya kipimo cha haimolojia ya mwili kwa Sh. milioni 14.045 badala ya Sh. milioni tano.

Hiyo ni mifano michache tu kwani taarifa ya Waziri Mkuu ilionyesha bayana kwamba katika taasisi hiyo iliyopewa jukumu la kununua na kusambaza dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya kuna udhaifu mkubwa katika eneo la ununuzi.


Kutokana na hali hiyo, Waziri Mkuu Kassim aliiagiza Bodi ya Wataalamu ya Ununuzi na Ugavi (PSPTB) kuwachukulia hatua waliohusika na vitendo hivyo pamoja na upotevu wa fedha za UVIKO - 19. Pia alitangaza kutembelea kesho MSD akiwa ameambatana na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupata maelezo ya kina juu ya wizi huo.

Vitendo kama hivyo pamoja na matumizi mabaya ya fedha kama ilivyoainishwa katika ripoti ya CAG havikubaliki hata kidogo kwa sababu vinaitia doa serikali. Kwa mantiki hiyo, vinapaswa kukomeshwa kwa wahusika kuchukuliwa hatua.

Kwa miaka mingi, CAG pamoja na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma wamekuwa wakitoa ripoti juu ya madudu hatua ambayo imekuwa kama utekelezaji wa wajibu wa ofisi hizo na kila mwaka madudu hayo yamekuwa yakiendelea kama kawaida.

Ni wakati mwafaka sasa kwa serikali kuwachukulia hatua wanaojihusisha na vitendo hivyo, si kwa kuwachukulia hatua kama ilivyoelekezwa kwa PSPTB kufuata kanuni za kitaaluma pekee, bali wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Marufuku hii isambae nchini kote kulinda afya za watu

**MTINDO** wa kuvuta sigara hadharani au kwenye mikusanyiko ya watu, umepigwa marufuku, kutokana na kile kinachoelezwa kuwa unahatarisha afya za watu wengine wasiotumia bidhaa za tumbaku.

Kanda ya Kati, imekuwa ya kwanza kupiga marufuku mtindo huo ambapo watumiaji wa bidhaa hizo wanatakiwa kutengewa maeneo maalum ambayo watayatumia kukata kiu yao bila kuathiri afya za wengine.

Ni maelekezo ya Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) Kanda ya Kati, Sonia Mkumbwa katika kikao kazi cha kutoa uelewa wa udhibiti wa bidhaa za tumbaku kilicho wakutanisha TMDA, uongozi wa wafanyabiashara na Viongozi wa ngazi ya mkoa na Manispaa ya Singida.

Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni huku akisema Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku kifungu cha 12(2), maeneo yasiyoruhusiwa kuwa ni pamoja na maktaba, sehemu za ibada na kambi.

Anataja maeneo mengine kuwa ni katika shughuli za michezo na burudani na sehemu zinazouza vyakula, ofisi, vyombo vya usafiri, mabanda ya maonyesho, masoko, maduka na sehemu nyingine za kukutania watu.

Aidha, anafafanua kuwa kwa mujibu wa sheria hiyo, mtu yeyote anayemiliki maeneo yaliyokatazwa anapaswa kutenga sehemu kwa ajili ya wavutaji, kwamba chumba kitakachokuwa kimetengwa kwa ajili ya uvutaji sigara kitatakiwa kuwa na mfumo wa kutolea moshi nje na kuweka maandishi ya 'No Smoking' na 'Hairuhusiwi kuvuta sigara katika maeneo pasiporuhusiwa.

Kimsingi, hatua hiyo ni nzuri inaweza kuokoa maisha ya wasiovuta, kwani imekuwa ni kawaida wavutaji kufanya hivyo hata kwenye mkusanyiko wa watu bila kujali kwamba wanaumiza wasiovuta.

Lakini pamoja na hilo, ninadhani ingekuwa ni vyema kama marufuku hiyo itakuwa ni kwa nchi nzima badala ya kuanzia Singida, huku watu wa maeneo mengine wakiendelea kuathirika kwa kuvutishwa moshi bila ridhaa yao.

Imekuwa ni kawaida kukuta mvuta sigara akivuta katika mikusanyiko mbalimbali ikiwamo ya abiria katika vituo vya mabasi, starehe au kwenye shughuli inayokusanya watu wengi bila hofu.

Wakati mwingine mzazi anaweza kuwa anavuta sigara huku akiwa amempakata mtoto wake, jambo ambalo pia wataalam wa afya wamekuwa wakielekeza kuwa ni hatari kwa anayevutishwa.

Hiyo inatokana na kile ambacho huwa kinaelezwa na wataalam hao kuwa anayevutishwa moshi wa sigara ana hatari ya kuumia na ndiyo maana huwa wanapendekeza kutengwa maeneo kwa ajili ya wavutaji wa tumbaku.

Nionavyo ni kwamba TMDA iangalie uwezekano wa marufuku hiyo kwenda sambamba na utoaji wa elimu nchi nzima, jamii iwe na uelewa wa kutosha kuhusu madhara ya tumbaku ili kulinda afya za wasiovuta.

Mwaka juzi, Wizara ya Afya ilisema kuwa asilimia 32 ya saratani husababishwa na tumbaku, kwamba katika kila wagonjwa 100 wanaobainika kuwa na saratani katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, 32 saratani zao zimesababishwa na utumiaji wa tumbaku.

Kwa hali kama hiyo, ni wazi kuna haja ya kuchukua hatua za makusudi kunusuru wale wanaovutishwa bila ridhaa yao, kwani inasemekana wanaovutishwa ndiyo wanaoumia zaidi.

Matumizi ya tumbaku yamekuwa yakitajwa kuathiri mfumo wa fahamu wa binadamu kwa kuwa kuna kichocheo kiitwacho nikotini ambacho kinafanya mtu ajione kama ana nguvu nyingi, hivyo kupenda kuitumia mara kwa mara.

## SAFU

### KWA MASLAHI YA TAIFA

# Mama Samia usiwaparue waparaji, ni wazuri kuliko wakunaji wazuri



Na Pascal Mayalla

MEI 3 kila mwaka huwa ni maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari. Nchini Tanzania, siku hii iliadhimishwa kitaifa jijini Arusha na mgeni rasmi alikuwa ni Rais Samia Suluhu Hassan.

Japo alisema mengi, kubwa lililonigusa ni hili la "Ukinikuna vizuri, mimi nakukuna huku nakupapasa na kukupuliza. Lakini ukinipara nakuparura! Naomba kuianza makala ya leo kwa kumkuna vizuri Rais Samia. Pongezi kwa Mama Samia, ndiye Rais wa Kwanza wa Tanzania kuwa mgeni rasmi Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari.

Niko chumba cha habari kwa kwa zaidi ya miaka 30. Hii ndiyo mara ya kwanza kwa tukio letu wanahabari kuhutubiwa na Rais wa nchi. Kiukweli kabisa, Rais Mama Samia ametuheshimisha sana. Asante sana Mama Samia, kutuheshimisha sisi wanahabari na sisi tunakuahidi kufuata kanuni ya 'reciprocity'. Ukiaminiwa, jiaminishe, ukiheshimiwa, jiheshimishe.

Kwa jinsi Rais Samia alivyotuheshimisha wanahabari, moja kwa moja na sisi wanahabari, tutamheshimu, tutamkuna vizuri ili atupapase na kutupuliza ufuu...., ufuu. Kwa vile Rais Mama Samia amethibitisha ana ngozi ngumu, ukitokea muwasho kwenye Magaga, hata ukune vipi, muwasho huo hauwezi kukunika ni lazima kumpara, hivyo ikitokea tumempara, tunamuomba sana Mama Samia, asituparure.

Pongezi zangu zisiishie kwa Rais Samia kutuhutubia, bali pongezi kwa vyama vyote vya Habari vikiongozwa na Jukwaa la Wahariri (TEF), Baraza la Habari Tanzania (MCT), MISA-Tan, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Muungano wa vyama vya habari vya mikoa Tanzania (UTPC) na waandishi wenyewe wa habari.

Pongezi mahususi kwa Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile na Mwenyekiti mstaafu Absolom Kibanda, kwa jitihada zao. Tena nilifurahi sana Rais Samia alipozungumzia SMS za Kibanda! Pongezi za tatu ni kwa Mama Samia, kukuza lugha yetu adhimu ya Kiswahili kwa kutuongezea misamiati mipya. Alianza na neno "kudemka", likaja neno "mkinizingua, tutazinguana", sasa ni neno "kupara". Msamiati wa Kukuna na Kupara. Kukuna ni kujikuna mahali panapokuwasha, Kupara ni kuchuna magamba ya samaki, Kupara samaki.

Kwenye kujikuna, mtu hawezi kujikuna mgongoni, hivyo mtu ukiwashwa mgongoni ni lazima umwombe mtu akukune na siku yeye akiwashwa nawe utamkuna. Kwenye kukuna kuna kumkuna mtu vizuri na kuna kumkuna mtu vibaya kama vile unampara samaki. Mama Samia katuasa sisi waandishi, tukimkuna vizuri, na yeye atatukuna vizuri, ila tukimpara atatuparua.

Kazi ya vyombo vya habari ni kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha, kukosoa na kuwajibika kwa jamii. Vyombo vya habari haviwajibiki kumkuna vizuri tu Rais, bali kwenye yale ya kustahili kumkuna vizuri, tutamkuna vizuri, ila yale yanayostahili kumpara, vyombo vya habari vina wajibu wa kumpara kwa lugha ya heshima na unyenyekevu mkubwa.

Kati ya vyombo vya habari vitakavyoandika habari za kumkuna vizuri tu Rais na vile vitakavyoandika habari za kumpara Rais, ni habari gani zitamsaidia zaidi Rais Samia na kulisaidia taifa? Kati ya mtu anayekusifu tu wakati wote na yule anayekusifu ukifanya lakini ukikosea anakukosoa na kukushauri, ni yupi atakusaidia zaidi?

Kwa lugha nyingine, wakunaji wazuri ni vile vyombo na wale waandishi ambao kazi yao siku zote itakuwa kumwandika vizuri na kumsifia tuu, halafu wapara ni vyombo au waandishi watakaomwandikia vibaya au kumkosoa.

Rais Samia naye ni binadamu na si malaika, hivyo kama binadamu ni haki yake kukosea, kwa sababu hakuna aliye mkamilifu isipokuwa Mungu pekee. Kwa mantiki hiyo, Rais kama binadamu, kuna mahali anaweza kukosea au amefanya ndivyo sivyo, hapo tupaseme si kwa kubeza au kukejeli, bali kufanyike kwa heshima, kwa lugha ya staha na unyenyekevu kwa lengo la kutoa ushauri wa kusaidia.

Kwa maana hiyo, ukosoaji kwa Rais ufanyike kwa nia njema ya kujenga na si kubomoa ili kumsaidia rais wetu kuwa Rais bora zaidi na kulisaidia taifa letu kusonga mbele badala ya kurudi nyuma. Nasema hivyo kwa sababu kwa mujibu wa katiba yetu, Rais hawezi kukosea ndiyo maana hawezi kushtakiwa.

Rais ana sehemu mbili, Rais ni taasisi, hivyo Rais kama taasisi hawezi kufanya kosa lolote. Kwa mantiki hiyo, kila kauli yake ni sheria, inafuatiwa na utekelezaji tu. Lakini hiyo taasisi inashikiliwa na kuongozwa na mtu ambaye ni binadamu tu kama sisi. Anayeitwa Samia Suluhu Hassan, huyu ni binadamu wa kawaida kama sisi wengine wote, hivyo anaweza kukosea.

Katika kumkosoa Rais, tumkosoe kwa heshima ili tusije kujikuta tunakosa uzalendo, badala ya kumkosoa, tunamuaibisha na kujikuta tunajiabisha sisi kama taifa. Naomba kauli hii ya Rais Samia, isitugawe wanahabari na jamii kugawanyika katika kambi mbili kuu, kambi ya kusifia na kambi ya kupondea. Kambi ya kusifia, wao kazi yao ni kusifia tu, hata kukifanyika mabaya au maovu kiasi gani, wao watasifu tu.

Kambi ya kuponda na kukosoa tuu, nao kazi yao ni kuponda, kupinga na kukashfu kila kinachofanywa na Rais Samia na serikali yake. Hata kiwe kizuri vipi, wao wataponda, watakosoa, watakashifu, watatukana , watadhalilisha na kubagaza. Mfano ni kazi nzuri ya filamu ya Royal Tour, kuna watu wanasifu, kuna watu wanaponda.

Na kundi la tatu ambalo ni dogo, hili lina watu 'very objective'. Wao Rais Samia na serikali yake, wakifanya mazuri, watampongeza na wakifanya mabaya, watamkosoa kwa kutumia 'constructive criticism'. Ukosoaji wao unafanyika kwa nia njema, si kwa lengo la kubeza, kukashfu, kudhalilisha au kubagaza.

Ukosoaji unaofanyika ni kwa nia njema kwa lengo la kusaidia, kutoa angalizo, kurekebisha na kutoa ushauri wa namna bora zaidi ya kufanya mambo. Ukosoaji wa aina hii, ni ukosoaji mzuri na ndiyo unaomsaidia Rais Samia na serikali yake kuliko wale wanaomsifia au wanaompondea tu.

Maadam Rais wetu Mama Samia, amekiri kwa kinywa chake kuwa ana ngozi ngumu na kuonyesha kwa dhamira, maneno na matendo, hivyo kwa niaba ya waandishi wenzangu wa habari, tunamwomba sana Mama Samia, kama atafurahia kukunwa vizuri, tunamwomba pia atuvumilie tukimpara na tunamwomba asituparure waparaji, kupara pia ni jukumu muhimu la vyombo vya habari.

**Wasalaam**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# LATRA fuateni nyazo za David Mwaibula



Na Joseph Kulangwa

TANGU Chifu Hangaya aifungue nchi kwa kuvuka mipaka na kwenda kwa wenzetu Ughaibuni na hasa la hivi karibuni la ziara yake ya The Royal Tour na kuhanikiza ujio wa watalii wengi kuna maswali mengi najiuliza.

Sawa tumekuwa tukipokea watalii kila siku, lakini hawatoshi kwani tunawahitaji kwa ajili ya kutuingizia fedha za kigeni, hivyo kwa Royal Tour ni dhahiri sasa watamwagika kama mafuriko ya mvua za masika.

Kuja watalii ni jambo moja lakini jinsi ya kuwapokea na kuwaonyesha ukarimu ni jambo lingine, hivyo Watanzania tunatakiwa kujiandaa na kukaa mkao wa kuhakikisha tunawapokea na wanapoondoka, wajisikie walikuwa nyumbani.

Ukarimu si lazima kumtabasamia mtu au kumpa chakula na maji ya kuoga, ni pamoja na wewe mwenyewe unavyoonekana, hasa katika usafi wako na jinsi hata mgeni akikusogelea, ajisikie anazungumza na binadamu mwenziwe, licha ya utofauti wa rangi.

Nalisema hili kwa kuangalia sisi Watanzania jinsi tunavyoishi maisha ya kubanduabandua na bila hata kujijali na kuonesha haiba yetu kwa wageni, ni jambo la kushangaza wakati mwingine.

Nataka kuchukulia eneo moja tu la usafiri hususan mijini, kwani mara nyingi kama si zote, watalii huanzia mijini kabla hawajajipanga kwenda nje ya miji kuangalia waliko wanyama kwani ndicho hasa cha msingi.

Nazungumzia hasa wenzetu wanaohudumu katika mabasi yanayobeba abiria mijini, maarufu kama daladala hususan jijini Dar es Salaam, ambako hivi sasa makondakta wanajivalia maguo machafu kama masulupwete.

Najiuliza kimetokea nini, kwani kuna nyakati makondakta na madereva walikuwa wakivaa sare, lakini leo ule utaratibu wa kila mtu kivyake umerejea na wanathubutu hata kuvalia mabukta machafu na hata 'Kata K'.

Hilo nadhani ni jukumu la Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) kuhakikisha usafi na utanashati kwa watu hawa, ambao baadhi yao pamoja na kuvalia nguo chafu huonekana hata maji wanayaogopa kama si sabuni kuwawasha!

Hivi ni nini kinashindikana kuwadhibiti watu hawa? Hivi LATRA inatwambia nini? Kama inashindwa kufanya hivyo huku huko nyuma kulikuwa na Mtanzania anaitwa David Mwaibula, ambaye alikuwa Jeshi la Mtu Mmoja akiwadhibiti watu hawa?

Kwa kweli katika enzi hizi za The Royal Tour kuwa na watu wa aina hii, ni kama nuksi fulani hivi, kwa sababu inaonesha hata katika taswira ya kimataifa kuwa Watanzania ni wachafu na isije wakafananisha tabia zetu na wanazozikuta mbugani kwa wanyama.

Haiwezekani na haiswihi kwa kweli, watumishi wa mabasi haya kuachwa wakiwa na uchafu wa aina hiyo na kupanda kwenye mabasi wakibanana na abiria wengine wanaokwenda kazini na katika shughuli zingine zinazohitaji utanashati.

Lakini kama hiyo haitoshi, hivi kwa nini LATRA inawaacha wenye mabasi haya wanajaza watu kama magunia ya vitunguu, wakibanana na kupumuliana hewa za juu na chini, kukoholeana na kupigiana chafya, kana kwamba hakuna korona?

Hivi nani alitangaza kuwa korona imetoweka hata kuruhusu sasa watu kubanana kwenye magari kiasi hicho cha kutia hata kinyaa? Pengine LATRA watoke watwambie ni kwa nini wanashindwa kusimamia sheria zao za udhibiti wa usafiri ardhini.

Naamini ni hao hao pia wanaosimamia bodaboda na bajaji, je, wanaridhishwa na utendaji wa watu waendeshao vyombo hivyo vya moto kweli, mpaka kuruhusiwa kuingia barabarani na kubeba abiria?

Ina maana LATRA ipo kwa ajili ya kutangaza nauli na si kufuatilia afya na usalama wa abiria katika vyombo hivyo na hata kusababisha wamiliki na watendaji katika vyombo hivyo kufanya wajuavyo wao.

Hebu LATRA tokeni nje piteni barabarani humo, angalieni nyendo za daladala, bodaboda na bajaji na mwone ni jinsi gani si kuwakamata lakini kuwaelimisha namna bora ya ustaarabu wa kufanya shughuli zao, ili ziwe rafiki kwa mwitikio chanya wa The Royal Tour ya Chifu Hangaya!

**Alamsiki!**

## Madiwani washtukia jambo anwani makazi

**Na Samson Chacha**

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Mji Tarime limemwagiza Ofisa Tehama aliyeshughulikia mchakato wa anwani za makazi maeneo hayo kuondoa vibao vilivyowekwa kwenye barabara za mitaa vyenye majina ya watu ambavyo havijafuata utaratibu wa serikali.

Agizo hilo lilitolewa juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Mji Tarime kilichofanyika chini ya Mwenyekiti wake, Daniel Komote na Mkurugenzi, Gwambina Ntovya na kuhudhuriwa na Mkuu wa Wilaya Tarime, Kanali Michael Mtenjele na Mwenyekiti wa CCM wilayani hapa, Daud Ngicho.

Kikao hicho kiliitishwa kujadili utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha miezi mitatu kilichoanzia Januari mwaka huu na kuangalia matatizo yaliyojitokeza. Miongoni mwa ajenda zilizojitokea ni hiyo ya anwani za makazi ambapo madiwani waliungana na wananchi kupinga utaratibu wa kuweka majina kwenye mitaa yao bila kufuata utaratibu.

Mwenyekiti Komote alisema: "Ninaungana na madiwani kupinga majina mapya yaliyowekwa katika mitaa yetu na kuondoa majina ya viongozi, waasisi na taasisi za umma na binafsi zilizokuwapo awali.

"Mfano, Mtaa wa Benki ya NMB iliyojengwa na kutoa huduma kwa muda mrefu na barabara hiyo inafahamika na watu wote, leo hii wanaondoa NMB wanaweka jina la Ghati Matunda, barabara zingine wameondoa majina ya waasisi na viongozi mashuhuri na kuweka majina ya watu ambao hawajajadiliwa na kutolewa uamuzi na wakazi wa mtaa husika." Komote alisema baraza limeazimia kumpa siku mbili Ofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) aliyeweka vibao hivyo, kuviondoa na kuacha vile vya zamani na wananchi maeneo husika wapewe nafasi ya kukaa na kupitisha.

"Tumepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuwa wapo baadhi wanadaiwa kununua mitaa badala ya kufuata utaratibu uliopo wa kujadiliwa, hii haikubaliki, lazima taratibu zifatwe," alionya.

Maagizo mengine yalitolewa kupitia kikao hicho ni walimu wakuu wawili wa Kata ya Turwa kutoka Shule za Msingi Buguti na Turwa kutakiwa kushushwa vyeo kutokana na kuwapo kwa malalamiko kukwamisha fedha.

"Mwalimu wa Shule ya Msingi Turwa amekwamisha fedha Sh. milioni 6.6 za ujenzi wa choo shuleni hapo na Kata ya Kenyamanyori kuna fedha za kukamilisha darasa zilitolewa na serikal Sh. milioni 25 zimekwama, baraza limeazimia hatua zichukuliwe kwa wahusika," Komote alisema.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Kanali Mtenjele aliwahimiza madiwani kufuatilia miradi ya maendeleo iliyopo katika kata zao na kuhakikisha fedha zilizotolewa zinakwenda na kutumika kama ilivyokusudiwa.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Tarime, Daud Ngicho, alisema mitaa mingi haina taa tangu zilizowekwa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tarime, Nyambari Nyangwine mwaka 2010.

# Wizara yaita wadau maoni maboresho sheria ununuzi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WIZARA ya Fedha na Mipango imetoa wito kwa wadau wa sekta ya ununuzi wa umma nchini kutoa mawazo kuwezesha maboresho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kuleta tija kwa serikali.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kamishna wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Frederick Mwakibinga, wakati akitoa elimu kuhusu sera, sheria, kanuni na miongozo ya ununuzi wa umma kwa washiriki waliotembelea banda la wizara hiyo katika wiki ya ununuzi wa umma jijini Arusha.

Alisema kuwa kuna sheria ya ununuzi wa umma sura 410 na kanuni zake ambayo kwa mara ya mwisho ilipitiwa mwaka 2013 na kanuni zake kutoka mwaka 2016.

"Tunaendelea kukusanya maoni kutoka makundi mbalimbali na watu wote ambao wanadhani nini kifanyike ili sheria iweze kutekelezeka na iweze kunufaisha nchi, hili ni jukumu letu kuhakikisha kuwa eneo la ununuzi wa umma lina sera, sheria, kanuni na miongozo inayokuwa na tija kwa Taifa," alisema Dk. Mwakibinga.

Alisema Sheria ya Ununuzi wa Umma inalinda maslahi ya Taifa kwa kuwa inawapa wananchi pamoja na wafadhili imani na serikali katika matumizi ya fedha, hivyo matumizi ya sheria hayapaswi kuingiliwa na mashinikizo.

Dk. Mwakibinga alisisitiza maofisa ununuzi nchini kusimama katika sheria, kufanya kazi kwa nidhamu, kuheshimu taratibu za ununuzi na kuepuka kukiuka matumizi ya sheria kutokana na shinikizo lolote na kuwasiliana na wizara endapo watakutana na shida ya shinikizo la aina yoyote.

Akizungumza kuhusu wiki ya ununuzi wa umma, alisema ni ya muhimu katika kuelimisha umma katika masuala mbalimbali ya ununuzi wa umma ili kufahamu umuhimu wake.

Alisema kuwa matumizi ya teknolojia katika ununuzi wa umma yanahakikisha eneo hilo linaendeshwa kwa kujali maslahi ya serikali na kushauri watendaji wote kuzingatia sheria, kanuni na kuzingatia maadili.

Washiriki waliotembelea banda la wizara hiyo walipongeza elimu inayotolewa katika wiki ya ununuzi wa umma na kutoa rai elimu kutolewa zaidi katika ngazi zote ili kuwezesha elimu hiyo kuongeza tija katika sekta ya ununuzi wa umma nchini.

Kongamano la Wiki ya Ununuzi wa Umma limeandaliwa na Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini ambazo ni Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA), Mamlaka ya Rufani za Zabuni za Umma (PPAA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB).



Mtaalam wa miradi wa Shirika la UNDP, Emmanuel Nko (kushoto), akitoa mada katika Mkutano wa Wiki ya Ubunifu Tanzania uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Austin Mkwaiya Makani Investment (AMMI), Austin Makani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Serikali yataka marekebisho kwenye miradi yenye dosari

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, ameziagiza Mamlaka za Mikoa na Wilaya kuhakikisha zinafanya marekebisho kwenye miradi ambayo imepitiwa na Mwenge wa Uhuru na kubainika kuwa na kasoro.

Katambi alitoa agizo hilo jana aliposhiriki mbio za Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Wilaya Kibaha mkoani Pwani.

Alisema miradi hiyo ambayo imekutwa na kasoro na kutolewa maelekezo na Mwenge, inatakiwa kufanyiwa marekebisho haraka kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa.

"Kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninazitaka mamlaka za mikoa, wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia maelekezo ya Mwenge wa Uhuru na kwenye maeneo ambayo miradi imekutwa na dosari kubwa, nisihi na kuitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wafuatilie miradi hiyo kwa haraka," alisema.

Aliongeza: "TAKUKURU wafanye ufuatiliaji wa haraka na kwa yale ambayo yatachukuliwa hatua, yafanyiwe hivyo ili miradi hiyo ianze kutoa huduma kwa wananchi."

Katambi alisema kwa maeneo ambayo Mwenge wa Uhuru bado haujafika, wahakikishe wanaandaa taarifa za miradi mapema pamoja na vipimo vinavyohitajika kwenye miradi hiyo.

Alisema Mwenge wa Uhuru kwa siku 36 tayari umepitia miradi 284 yenye thamani ya Sh. bilioni 69.2 hadi kufikia Mei 6 mwaka huu.

Alisema shughuli za Mwenge wa Uhuru hazitakiwi kufanyiwa mzaha kwa kuwa upo kutekeleza adhma yake, falsafa na sababu ya kuenziwa kwa kuhakikisha kile kinachofanywa kwenye miradi ya maendeleo ni kile walichotumwa na Rais.

Katambi alisema kazi kubwa wa Mwenge wa Uhuru ni kusimamia utawala bora, kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo ambayo serikali inatumia fedha nyingi kuhakikisha inatoa huduma kwa wananchi.

Aliwapongeza wakimbiza Mwenge kwa kukagua miradi ya maendeleo kwa kiwango kinachotakiwa huku akiendelea kuwasisitiza kuzingatia maelekezo katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Awali, akitoa taarifa ya miradi inayotembelewa na Mwenge wa Uhuru katika halmashauri hiyo, MKuu wa Wlaya ya Kibaha, Sara Msafiri, alisema miradi 12 yenye thamani ya Sh. bilioni 2.2 itatembelewa.

# MAISHA

MEI 8, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

JICHO LENYE BASHASHA

## Tumia vyakula kuondoa weusi




Ukurasa 15

MAISHA NI NYUMBA

Dondoo namna ya kusafisha jiko la gesi



Ukurasa 12

HARUSI




# Toka na kipara

Ukurasa 13


## WATOTO

MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | J | E | M | B | E |
| ■ | A | ■ | ■ | O | ■ |
| U | M | A | ■ | N | ■ |
| ■ | B | ■ | I | G | A |
| ■ | I | ■ | ■ | E | ■ |
| J | A | N | G | A | ■ |





## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
TBC, DOA, DONDA, MKUKI, MSONDO, KIMBIA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Anna alikuwa akimsaidia mama yake kazi za nyumbani ikiwamo kusafisha eneo la jikoni. Wakati akisafisha sakafu mara muuza bidhaa mbalimbali za ndani aligonga mlango.

Anna alikwenda kufungua mlango na kumkuta muuza bidhaa akiwa amesimama na kumuuliza kama mama yake yupo. Anna alijibu hayupo, kisha alirudi haraka kwa mama yake kwenda kumwambia.

**Anna:** Mama yule muuza bidhaa alikuja, lakini nikamwambia haupo

**Mama:** Kwa nini mwanangu?

**Anna:** Mwalimu alituambia kuwa 'kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza'. Sasa yule anatembeza vitu.

**Mama:** Hapana huo ni msemo tu ukimaanisha kila kitu kizuri kinaonekana haraka, lakini sio haiwezekani kutembezwa kuuzwa.

**SWALI**

Mnyama Chui yuko katika jamii gani ya wanyama?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Wivu, choyo vichocheo vya kuua imani ndani yako

***KARIBU tena msomaji tumalizie sehemu ya mwisho ya mada yetu kuhusu mambo yanayoua imani ya watu wengi. Tayari nimejadili kuzoea hali ya kushindwa, kutegemea nguvu na akili zako na kuendekeza roho ya mashaka na woga.***

Katika roho ya mashaka nikasema kwamba roho hii haitoki kwa Mungu, maana neno lake linasema, "Maana Mungu hakutupa roho ya woga bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi".

Nikaeleza kwamba hakuna mtu anayeweza kufanikiwa katika maisha kama bado anaburuzwa na roho ya mashaka na woga. Mapacha hawa hukufanya usimwamini Mungu. Matokeo ya kutomwamini Mungu na kuendekeza mashaka na woga, Mungu anasema hivi katika neno lake;

“Wala katika mataifa hayo hutapata raha iwayo yote, wala hutakuwa kituo cha wayo wa mguu wako; Lakini Bwana atakupa huko moyo wa kutetema na macho ya kuzimia na roho ya kudhoofika na uzima wako utakuwa na wasiwasi mbele yako; nawe utakuwa na woga usiku na mchana, wala hutaamini kamwe maisha yako...”

Sasa tuingie kipengele kingine cha wivu na pacha wake uchoyo. Ni vigumu sana kujitambua kwamba una tatizo la wivu. Ni kawaida sana kuona wengine ndio wanaokuonea wivu. Wivu hujulikana pia kama husuda au gere, yaani hali ya kukerwa au kukosa amani unapoona wengine wanafanikiwa!

Mtu mwenye wivu hasemi jambo jema kuhusu mwenzake. Mtu akijenga nyumba au kununua gari hatakosa cha kulaumu. Jipime na ukiona huwezi kusifia maendeleo ya wengine toka moyoni, utakuwa unasumbuliwa na roho ya wivu.

Wivu ni sumu inayoua imani yako na hatimaye kuiondoa kabisa. Unapowaonea wengine wivu, maana yake unamlaumu Mungu kwa kukusahau na kutokuweza kukufanikisha. Ukiendekeza hali hii, mawasiliano na Mungu yatakatika na Lucifa (shetani), mwenyewe atachukua usukani wa maisha yako. Lucifa ndiye mwasisi wa wivu alitamani kuwa kama Mungu!

Wivu huzaa tamaa na tamaa huzaa mauti. Sambamba na wivu, choyo ndiye mshirika wake mkubwa. Unapowaonea wivu waliofanikiwa, unajenga tabia ya kulinda kile ulicho nacho kwa sababu unaona kama Mungu amekuacha.

Hali hii huitwa uchoyo! Yaani kujiona umepungukiwa kila wakati na kusahau maneno ya Mungu ya mtunga zaburi; “Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu”. Kama ulivyo kwa wivu ni ngumu kujiona una roho ya uchoyo. Jipime kama kila unapotakiwa kusaidia au kutoa kitu unajitetea kwamba huna; huo ni uchoyo. Hakuna mtu mwenye roho ya uchoyo akamwamini na kumtegemea Mungu na hawezi kufanikiwa katika maisha. Choyo hufunga baraka za Mungu kwako!

Pia kauli za kushindwa huua imani. Watu wengi hawaelewi kwamba kile kinachotoka kinywani ndicho kilichojaa moyoni mwa mtu. Ukitamka kushinda au kushindwa ndicho kilichojaza moyo wako kwa sababu ndicho unachoamini. Neno la Mungu linasema, “bali vitokavyo kinywani vyatoka moyoni; navyo ndivyo vimtiavyo mtu unajisi”.

Kauli ya mtu inapata nguvu yake katika lile analoliamini, kile unachokiri kwa kinywa kinaumbika na kutokea kuwa halisi katika maisha yako. Ulimi una nguvu kwa sababu unawakilisha imani iliyo ndani yako. “Mauti na uzima huwa katika uweza wa ulimi; na wao waupendao watakula matunda yake”.

Ukitaka kuimarisha imani itendayo kazi maishani mwako, jenga tabia ya kukiri ushindi kila wakati hata kama mambo yako hayaendi vizuri. Mungu aonapo imani yako, hatimaye atakukirimia haja ya moyo wako !

Wapo watu kazi yao ni kuzungumzia shida tu. Atakuelezea jinsi ambavyo mambo yake yanavyomwendea vibaya. Inawezekana ni kweli yanayomkuta lakini asichofahamu ni kwamba hali hiyo ni matokeo ya kile anachokiri kwa kinywa chake kila wakati. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Mungu anasisitiza kwa kusema, “Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna”.

Haiwezekani kila wakati unazungumzia jinsi biashara, ndoa, afya yako inavyokwenda vibaya halafu utarajie mafanikio! Mtu wa aina hii haenendi kwa imani, bali kwa kuona na kila wakati anaona shida.

***Mpenzi msomaji, Tuonane wiki ijayo. Naamini umeweza kujifunza kitu kuinua kiwango cha imani katika maisha yako! Je, una maoni? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Royal Tour imeshazinduliwa, kazi kwetu kutumia fursa hii

WIKI mbili zilizopita katika safu hii, niliandika juu ya umuhimu wa kutumia filamu ya Royal Tour kujitangaza na kujiimarisha kiuchumi kupitia fursa mbalimbali zilizopo nchini ikiwamo utalii.

Filamu hiyo ambayo ilichezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa kama mwongoza watalii akimwongoza Mwandishi Peter Greenberg, ambaye alitembezwa na kuelezwa kwa kina kuhusu vivutio vilivyoko nchini, imeshazinduliwa rasmi na Rais wiki hii jijini Arusha.

Katika kuhakikisha filamu hiyo inatumika ipasavyo, jana ilikuwa zamu ya Zanzibar kuizindua huku mgeni rasmi akiwa Rais Hussein Mwinyi. Leo ndiyo leo kwa wakazi za Dar es Salaam kushuhudia tukio kama hilo ikiwa ni hatua ya kuipa ‘mileage’ zaidi.

Kwa kifupi, katika filamu hiyo, Rais Samia anaonekana kumudu vyema kazi yake ya kuongoza watalii kwa kumweleza kuhusu vivutio kwenye Hifadhi za Taifa na vivutio vilivyoko Zanzibar. Yote hayo ni kuutangazia ulimwengu kwamba Tanzania ina vivutio kedekede kwa ajili ya utalii pamoja na rasilimali ambazo zikitumiwa ipasavyo, zitaifanya Tanzania kuwa tajiri tofauti na inavyofikiriwa au kueleweka katika jumuiya ya kimataifa.

Ukitazama sehemu ndogo ya filamu hiyo iliyoachiwa kwenye mitandao utaona namna gani inatengeneza hamu au sababu ya mgeni kutoka taifa lolote anapopanga safari yake kufikiria pa kwenda ni Tanzania pekee na siyo kwingine.

Mara nyingi tumeona jitihada za nchi jirani kujitangaza kwa kutumia vivutio vilivyopo nchini mwao hata vile vilivyopo mpakani wanavitumia ili kuwavutia watalii.

Mathalani, niliwahi kwenda Geneva, Uswisi nikaona mabasi na treni kwa wiki moja ambayo kulikuwa na mkutano wa dunia wa masuala ya majanga, yakiwa yamepambwa picha za Mlima Kilimanjaro, hifadhi za taifa na wanyama watano wakubwa wanaopatikana nchini humo. Lengo kubwa ni kutengeneza sababu kwanini mtalii atembelee kwao.

Nilivyofika uwanja wa ndege niliona kwenye mbao za matangazo za ndani na nje wameweka Mlima Kilimanjaro na wanyama hao, kuendelea kumshawishi mtalii kupanga safari na kuifanya nchi hiyo kuwa kituo chake muhimu.

Ndani ya ndege ya Shirika la Ndege la Uturuki, nilikuta jarida ambalo ndani yake kulikuwa na makala iliyoandikwa kwa ustadi ikiambatanishwa na picha mbalimbali, kuendelea kutengeneza sababu ya mtalii kwenda nchini humo.

Kama Mtanzania nilisikitika kwa nini sikuona makala ya nchi yangu wakati naelewa fika Mlima Kilimanjaro uko nchini kwangu. Ukitaka kuupanda vizuri kwa njia nzuri na kuuona vizuri lazima upandie Tanzania, lakini ukitaka kuona nyumbu wanavyohama lazima uje upande wa Tanzania.

Kama haitoshi nyumbu wote wana hati za kusafiria za Tanzania, kwa kuwa lazima wakabebe mimba Masai Mara waanze kurudi taratibu wakipita kituo hadi kituo ikiwamo eneo la mtawanyiko Loliondo, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na baadaye kurudi Hifadhi ya Taifa Serengeti ambako huzaliana. Ikiwa kutakuwa hakuna mvua basi wanauwezo wa kuahirisha kuzaa hata kwa miezi mitatu.

Hatimaye yaliyokuwa yakionekana katika nchi za wenzetu yamekuja sebuleni kwetu. Filamu ya Royal Tour ni muhimu kwa taifa letu kwa maana ya sekta binafsi na serikali. Ninasema hivyo kwa sababu itasaidia kukuza uchumi wa nchi yetu kutokana na kutangaza vivutio vyetu, hivyo kuwafanya watalii kumiminika kwa wingi nchini.

Watalii wanapoongezeka kwenye hifadhi na vivutio vyetu ndipo mapato, ajira za kudumu na huduma za kijamii zinaongezeka. Wawekezaji watajenga hoteli hivyo watahitaji watu wa kuajiri, watanunua bidhaa kutoka kwa wakulima, wananchi watauza bidhaa za utalii au zinazoendana na utalii kama vitu vya utamaduni, vyakula vya asili na kuonyesha utamaduni wao na hatimaye kujipatia kipato.

Pia kuna maeneo yaliyohifadhiwa na jamii yanayojulikana kama Wildlife Management Areas (WMA),ambayo wanyama hupita kwenda hifadhi nyingine, wanajipatia kipato kwa kuwa na wawekezaji.

Katika kila hifadhi kuna ujirani mwema, kwamba sehemu ya mapato yanarudi kwa jamii kupitia vipaunbele vyao vya huduma za kijamii kama shule, hospitali na miundombinu ya maji na barabara ambavyo ni kwa faida yao.

Kwa ujumla kwenye utalii kuna ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, hivyo filamu hii itakapoanza kuleta matokeo ni lazima tuyatumie vizuri kwa manufaa yetu binafsi, maeneo yetu na taifa kwa ujumla.

Lazima kila mmoja katika eneo lake ikiwamo sekta binafsi kujiandaa kunyonya fursa zilizopo. Tufanye hivyo kwa kutumia fursa ya uwapo wa filamu ya Royal Tour kuchangamkia neema itakayokuja kwa watalii na wawekezaji kuingia nchini na kutembelea vivutio hivyo na hatimaye kupata ahueni ya maisha.

Hata hivyo, nitoe angalizo tu kwamba baadhi ya watu wameanza kubeza kazi hiyo nzuri iliyofanywa na Rais Samia ambaye kwa dhati ameonyesha kuwa anataka kuifikisha Tanzania katika neema kwa kuibua vitega uchumi na kutangaza vivutio vyetu. Niseme wazi kwamba watabeza na ndiyo desturi yao lakini tuendelee kutumia fursa hii ili watakapokuja kubaini umuhimu wake, watakuwa wamechelewa.

**“Mara nyingi tumeona jitihada za nchi jirani kujitangaza kwa kutumia vivutio vilivyopo nchini mwao hata vile vilivyopo mpakani wanavitumia ili kuwavutia watalii.**

# HARUSI





Ndoa ya mtangazaji wa Wasafi Radio na mume wake Shekhe Abdulrazak Salum, imetimu mwezi mmoja wakiwa katika mahaba mazito. Je watakuwa mfano bora wa kudumu muda mrefu kama watu maarufu wanaofuatiliwa?









# MITINDO





# Toka na kipara

SUALA la mitindo linawagusa moja kwa moja wanawake na wanaume ambao kila siku wanapenda kuwa na mwonekano mzuri na kujiamini.

Ukiacha mavazi na mapambo, mitindo ya nywele imekuwa na mapana yake pale mtu anapotaka kuwa tofauti.

Mtindo wa kunyoa nywele zote maarufu 'kipara' umeonekana kuwavutia vijana wengi wanaohitaji kuwa watanashati zaidi.

Wataalamu wa masuala ya mitindo wanasema watu wanaopenda kunyoa nywele zote mara nyingi wanaonekana watanashati zaidi mbele ya jamii.

Hata hivyo mtindo huo hauna gharama kubwa na hivyo kuwafanya watu kupunguza presha ya maisha.

**UTATOKAJE NA KIPARA?**

Aina hii ya mtindo hauna gharama ya ukataji wa nywele, mara nyingi nywele zikiondolewa unatakiwa kupaka mafuta maalum ya kuhifadhi ngozi. Inapendekezwa mafuta ya asili kama ya nazi au mzaituni yanafaa kupaka.

Hata hivyo, mtu anakuwa huru zaidi kufanya kila jambo kwani hutumia muda mfupi kujiandaa au kujipodoa pale anapotaka kutoka.

Mara nyingi ukiwa na 'kipara' unapendeza kuvaa nguo aina yoyote na kwenda sehemu yoyote ile bila kupata bughudha au kukiuka sheria.

UREMBO



JICHO LENYE BASHASHA

# tumia vyakula kuondoa weusi

TATIZO la kuwa na rangi nyeusi chini ya macho ni hali inayoweza kumpata mtu yoyote na katika umri wowote.

Zipo sababu zinazosababisha mtu kupata weusi kwenye macho zikiwamo za urithi ambayo unazaliwa nayo pia matumizi ya vipodozi vyenye kiwango kingi cha kemikali na mabadiliko ya homoni ndani ya mwili.

Nyingine ni kuwa na mawazo sana, kukosa muda wa kutosha wa kupumzika, kuvaa miwani muda mrefu na maisha ya mtu husika.

Unatakiwa uelewe kwamba weusi chini ya macho ni tatizo na usipochukulia hatua vizuri linaweza kuwa kubwa kwa afya yako.

Kama wewe ni mmojawapo wa wenye tatizo hili bado una nafasi ya kutibu na kuirutubisha ngozi yako ya jicho kama hapo awali.

**TUNGULE NA NDIMU**

Juisi ya tungule na ndimu husaidia kuondoa weusi na hata kuifanya ngozi yako iwe laini na sio laini sana.

**JINSI YA KUANDAA**

Kata ndimu yako robo kipande na tungule nusu kipande, changanya pamoja.

Kisha paka chini ya macho. Acha ikae kwa dakika 20, kisha nawa kwa maji safi. Fanya hivi mara mbili kwa siku asubuhi na jioni

**MBATATA KILICHOSAGWA**

Chukua kiazi na kisage vizuri ili upate juisi yake. Tumia kitambaa safi au pamba kupaka juisi yako ya mbatata chini ya jicho, unaweza pia kuzungushia jicho. Acha kwa dakika 20 kisha nawa kwa maji safi

**MAJANI YA CHAI**

Chukua majani ya chai yaliyowekwa katika karatasi maalum maarufu kama 'tea bag' mbili zinazoweza kuwa za green tea au chamomile na uweke katika maji, kisha weka ndani ya friji kwa muda wa saa moja.

Toa kisha weka juu ya macho yako, kaa nayo kwa muda wa dakika 20, kisha nawa kwa maji safi.

Unaweza kufanya hivi kila siku hadi pale utakapoanza kupata matokeo mazuri.

**MAZIWA AU MTINDI BARIDI**

Chukua pamba au kitambaa na udumbukize katika kibakuli kilichowekwa kiwango kidogo cha maziwa au mtindi, kisha paka chini ya macho au unaweza kuzungushia jicho zima. Kaa kwa dakika 20 kisha nawa kwa maji safi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia vitumbua vya mayai

VITUMBUA ni baadhi ya vitafunwa vilivyozoeleka kutumia mchele pekee, lakini mayai hutumika pia kuongeza ladha.

**Jinsi ya kuandaa**

Kikombe kimoja cha mchele, kijiko cha kulia cha unga wa ngano, kikombe cha tui la nazi zito na mayai.

Mahitaji mengine ni kijiko kimoja cha chai cha hamira, sukari nusu kikombe na hiliki kiasi upendacho.









**Namna ya kuandaa, kupika**

Osha na kuloweka mchele ndani ya maji ya baridi saa nane au siku moja.

Mimina vyote isipokuwa sukari, ndani ya blender na usage mpaka mchele uwe umesagika kabisa.

Mimina sukari ndani ya mchanganyiko na usage tena kidogo tu.

Mimina mchanganyiko ndani ya bakuli na ufunike. Weka bakuli mahali penye joto ili mchanganyiko uumuke.

Mchanganyiko ukisha umuka, weka karai kwenye moto.

Tumia kama kijiko kimoja au viwili vya chai cha mafuta kwa kukaangia kila kitumbua.

Mimina mchanganyiko kiasi kwenye karai kulingana na kikarai unachotumia.

Kitumbua kikiiva upande mmoja, geuza upande wa pili mpaka kiwe tayari.

Panga kwenye sahani na unaweza kula vitumbua vikiwa moto au vikipoa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Fanya uchaguzi sahihi wa sakafu ya nyumba

KILA uchao tunashuhudia mabadiliko yanayojitokeza maishani ambayo kwa namna mbalimbali yanasababishwa na maisha ya utandawazi tuliyo nayo katika karne ya leo.

Mambo yaliyofanyika jana si yale yatakayofanyika kesho wala keshokutwa. Kila siku yanaibuliwa mapya au kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi endapo yaliwahi kufanywa. Na leo tunaangalia ubora uliopo sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba.

Katika nyumba, sakafu ni moja ya vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba na hata pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

Yako baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba ambayo Msanifu Majengo, Peter Lameck, anaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane sana.

Jambo la pili ambalo anasema linapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake.

Jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba yako.

"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa, maana nyingine zina utelezi mkali," anasema Lameck.

Jambo la nne, anasema ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anasisitiza.





Na jambo la tano, anashauri kwamba ni vema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.

## Namna kusafisha jiko lako la gesi



KATIKA kuhakikisha jiko lako la gesi linakuwa safi, unatakiwa kuwa makini katika kuliweka kwenye nazingira mazuri.

Pamoja na matumizi yake ya haraka na kukupatia mlo kwa wakati, lakini usafi ni jambo la muhimu unalotakiwa kulizingatia.

Kuna njia tofauti za kusafisha jiko la gesi, hata hivyo unatakiwa kuchagua moja ambayo unaona inafaa na gharama nafuu.


**1:** Sabuni ni njia mojawapo rahisi na hukupatia matokeo mazuri wakati wa kusafisha jiko lako.Unahitaji kusugua kwa sabuni na uifute kwa lita saba za maji ya moto.

**2:** Amonia... Njia isiyo na gharama kubwa, nunua chupa moja katika duka la dawa, lakini wakati wa kuitumia, ni muhimu kulinda kwa vifaa maalum.

**3:** Soda gruel inafaa zaidi kusafishia jiko, lakini kuweka, changanya kiasi sawa cha soda na maji.

**4:** Siki na soda pia inatumika kusafishia jiko. Unatakiwa kuchanganya mapema kabla ya kusafisha. Njia hii ni bora zaidi na hung'arisha jiko.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
KIVAZI HIKI ALAFU MAFUTA YAMEPANDA, GARI TUSHAIFUNGIA... TUKIKUTANA NA PANYARODI?
EBO! NILIDHANI UTATHEMA TUKI-KUTANA NA 'MKWE WANGU!'
WEWE KAZI YAKO NIONESHE KILA NYUMBA YENYE 'PANYARODI' KISHA NIACHIE MIMI NITADILI NAO
UHATHAMA HUO! NIKISHAKUONESHA UNADHANI WADHADHI WAO WATANIPIGIA KURA UCHAGUDHI UJAO? NIJIBU...
JOMBO LA DORA
MWENE-KITI MTAA
KUNA KUNDI LA VIJANA WANA-MAPANGA NA MARUNGU
NA MIMI NIMESHIKA NINI?
WE'BWANA KUOMBANA LIFTI MWISHO LEO, MAFUTA YAMENIKAMUA HELA PALE SHELI HATA POLE IMEKUSHINDA!
NI KWELI SURA ILIKUWA KAMA UNAMINYWA JIPU BICHI!
NASIKITIKA SINA NDOGONDOGO NINA KUBWA TUPU!
USIJALI UKUBWA WAKE NITWISHE UONE!
MWANAUME GANI HELA HUTOI MPAKA UHESABIE MFUKONI
SAMTAIMU NAHESABIAGA CHOONI HADI HARUFU NIME-IZOEA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MCHEZO WA MAPENZI HAUNA REFA

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani kupeleka shehena nyingine ya silaha Ukraine



Baadhi ya ria wa Ukraine wakiokolewa kutoka kiwanda cha chuma cha Azovstal mjini Mariupol juzi. **PICHA: DW**

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden ametangaza shehena mpya ya silaha yenye thamani ya Dola milioni 150 kwa ajili ya kuisaidia Ukraine kupambana na Russia.

Kwa mujibu wa ofisa mwandamizi wa nchi hiyo, alisema shehena hiyo inajumuisha risasi 25,000, rada za kutambua sehemu zilipo silaha za adui pamoja na vipuri.

Kabla ya tangazo hilo lililotolewa juzi, utawala wa Biden tayari ulikuwa umeshatuma shehena nyengine ya silaha zenye thamani ya zaidi ya Dola Bilioni 3.4 kwa Ukraine.

Shehena hiyo mpya inamaanisha kuwa kiasi cha Dola milioni 250 zilizoidhinishwa awali ili kuisadia Ukraine zimekwisha.

Biden analishinikiza bunge la Marekani kuidhinisha msaada mwengine wa Dola bilioni 33 kuisaidia Ukraine, ikiwemo Dola bilioni 20 za usaidizi wa kijeshi.

Rais huyo na viongozi wengine wa kundi la mataifa saba yenye uchumi mkubwa duniani G7 pamoja na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, wanatarajiwa kufanya mkutano kwa njia ya mtandao leo kujadili uungwaji mkono wa nchi za Magharibi katika mapambano yao dhidi ya Russia.

Biden alisema katika taarifa yake kuwa Marekani imetoa kiasi kikubwa cha fedha ili kuisaidia Ukraine haraka iwezekanavyo. "Tunatuma silaha na vifaa vingine muhimu ambavyo bunge la Congress lilikuwa limeidhinisha." Alisema Biden

Kiongozi huyo hata hivyo alisema ufadhili huo unakaribia kuisha, na kwamba iwapo Ukraine itakuwa na fursa yoyote ya kufanikiwa katika vita vyake dhidi ya Russia, basi Marekani na washirika wake wanapaswa kuipiga jeki kwa kuipelekea silaha.

Watu zaidi waokolewa kutoka mji wa Mariupol

Makumi ya watu wameokolewa kutoka kiwanda cha chuma kilichozingirwa ambapo wapiganaji wa Ukraine waliopo mjini Mariupol wamekuwa wakipambana kuzuia vikosi vya Russia kuchukua udhibiti kamili wa mji huo.

Maofisa wa Russia na Ukraine wamesema watu 50 wameokolewa kutoka kiwanda cha chuma cha Azovstal na kukabidhiwa kwa wawakilishi wa Umoja wa Mataifa na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu.

Jeshi la Russia limesema, watu 11 kati ya waliookolewa ni watoto.

Maofisa wa Russia na Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine, Iryna Vereshchuk, walisema zoezi la uokoaji lingeendelea jana .Watu hao waliookolewa wanajumuisha wengine wapatao 500 kutoka mji wa Mariupol siku za hivi karibuni.

Kulingana na makisio ya Russia, takriban wapiganaji 2,000 wa Ukraine, wamejificha kwenye mashimo ya chini kwa chini karibu na kiwanda cha chuma cha Azovstal, na kwamba wamekataa miito ya kujisalimisha.

**RAIS WA UKRAINE ACHORA MSTARI MWEKUNDU**

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amesema raia wake 50 hawakuweza kuondolewa kwenye mji wa viwanda vya chuma wa Mauripol siku ya Ijumaa.

Mji huo tayari umedhibitwa na majeshi ya Russia katika mapigano yanayoendelea nchini humo.

Kiongozi huyo, alisema kama kuna mpango wowote wa amani na Russia, basi utategemea kurudi nyuma kwanza kwenye maeneo vilipokuwa vikosi vyao kabla ya uvamizi.

Akizungumza na bodi ya washauri wa masuala ya kisiasa na uchumi mjini London, Rais Zelensky, alisema kwamba hicho ndicho kigezo cha chini anachoweza kukubali.

Alisema amekuwa kiongozi wa 'Ukraine, na sio Ukraine nusu . Lakini hakuitaja Crimea, jimbo lililotwaliwa na Russia katika mwaka 2014.

Russia kwa sasa inapigana kuchukua udhibiti kamili wa mji wa Mariupol.

Bado kuna vikosi vya Ukraine pamoja na baadhi ya raia kusini -mashariki mwa mji wa Azovstal , ambao umekumbwa na mashambulizi makali kutoka Russia.

Kuuteka mji wa Mauripol itakuwa ni mafanikio makubwa zaidi katika kipindi cha miezi miwili ya vita na itampa Rais wa Russia Vladimir Putin kitu fulani cha kusherehekea siku ya ushindi ya nchi hiyo kama kumbukumbu ya ushindi wa katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

**WABELARUS WALICHANGIA KUIRUDISHA NYUMA RUSSIA**

WATU wanaoipinga serikali ya Belarus, walikuwa na mchango mkubwa katika kuilazimisha Russia kuachana na jaribio lake la kuteka mji mkuu wa Ukraine, Kyiv.

Kiongozi wa upinzani wa Belarus, Svetlana Tikhanovskaya, aliambia BBC kuwa kulikuwa na vitendo 80 vya njama za hujuma dhidi ya leri ambayo ilitumiwa kuwapelekea silaha wanajeshi wa Russia kabla ya kuondoka kaskazini mwa Ukraine mwezi mmoja uliopita.

Alisema wanaharakati walikuwa wanatoa taarifa za ujasusi kuhusu matembezi ya wanajeshi na ufyatuaji wa makombora.

Wabelarus zaidi ya asilimia 86 walikuwa hawaungi mkono vita hiyo.

Tikhanovskaya alisema hatma ya Ukraine na Belarus inaunganishwa na ushindi unaoweza kuisaidia nchi yao kuwa huru na utawala wa kiimla wa Alexander Lukashenko.

Baadhi ya vikosi vya Russia viliingia nchini Ukraine vikitokea Belarus, ambavyo inaonekana kama taifa lenye ushirika na Russia.

**BBC**

## Mlipuko waua 22, wateketeza hoteli maarufu

**HAVANA, Cuba**

WATU 22 wamefariki na wengine zaidi ya 60 wamejeruhiwa baada ya mlipuko mkubwa kutokea katika hoteli ya kifahari nchini Cuba.

Inaaminika kuwa mlipuko huo ulitokana na tanki la gesi liloegeshwa nje ya hoteli hiyo inayoitwa Saratoga, iliyopo katika eneo la Old Havana.

Kabla ya mlipuko huo, tanki hilo liliwaka moto na kisha kusababisha mlipuko ambao uliharibu magorofa kadhaa ya jengo.

Hoteli hiyo ya kihistoria ilikuwa imejiandaa kwa ajili ya kufunguliwa baada ya janga la Covid katika kipindi cha siku nne zijazo.

Mlipuko huo umeacha hoteli hiyo kuwa magofu, huku sehemu kubwa ya kuta zake za nje zikiwa zimepasuka.

Operesheni ya msako na uokoaji iliendelea kuwatafuta watu waliokwama chini ya vifusi vya jengo.

Rais wa Cuba alisema miongoni mwa watu waliokufa ni pamoja na mwanamke mmoja mjamzito pamoja na mtoto.

**BBC**

## MAKALA

# BARUA YA WAZI KWA SPIKA WA BUNGE LA TANZANIA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

NDUGU Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kutumia haki yangu ya kikatiba kwa mujibu wa ibara ya 18(1) inayosema “Bila ya kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi.” Natambua kuwa ibara ya 63(2) ya Katiba yetu inalipa mamlaka bunge lako tukufu kuwa chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano kuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi katika kuishauri na kuisimamia serikali pamoja na kutunga sheria kama ilivyoainishwa katika ibara ya 64(1).

Hivyo basi, napenda kutoa maoni au mchango wangu kuhusu “Mapendekezo ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba saba ya mwaka 2021 ya mwenendo wa makosa ya jinai kifungu cha 131A kinachopendekeza kuwekwa masharti ya kutoshtakiwa mtuhumiwa hadi pale upelelezi utakapokuwa umekamilika.”

Kwanza nikiri kwamba mimi si mtaalam sana wa sheria na kama nitakuwa nimeelewa vizuri, jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa zaidi ni juu ya mtu kukamatwa na kuwekwa ndani kabla ya upelelezi kukamilika, kitendo kinachofanya watu wengi kuwa ndani kwa kipindi kirefu huku wakiambiwa upelelezi unaendelea.

Si jambo la kushtakiwa pekee kwa sababu mtu anaweza kushtakiwa ama akiwa nje au akiwa ndani. Unaweza kukamatwa ukashitakiwa kama upelelezi umekamilika au ukakamatwa usishitakiwe kwa sababu upelelezi unaendelea huku ukiwa unasota mahabusu.

Kwa hiyo, kwanza nakubaliana na mapendekezo hayo, kwa sababu ni jambo litakalosaidia kupunguza idadi ya watu katika magereza yetu na kuipunguzia mzigo mkubwa serikali wa kuwahudumia mahabusu. Lakini pia jambo la kukamatwa na kuwekwa ndani bila upelelezi kukamilika linawapotezea muda watuhumiwa ambao baadaye wanakuja kujulikana kuwa hawana hatia mbele ya sheria na bahati mbaya hawafidiwi muda wao walioupoteza wakiwa magereza pamoja na kuharibiwa taswira yao katika jamii.

Ndugu Spika, pamoja na mapendekezo hayo yenye nia njema kabisa, najaribu kujiuliza maswali kadhaa, mapendekezo ya mswada yanataka mtuhumiwa asishitakiwe mpaka upelelezi utakapokamilika. Swali la kwanza, wakati upelelezi unaendelea huyu mtuhumiwa atakuwa wapi muda huo? Je, sheria na mazingira vitawalindaje mtuhumiwa pamoja na mpelelezi wasiwasiliane? Kama tafsiri ya muswada huu itakuwa ni kufanyika upelelezi mtuhumiwa akiwa huru ni kwa namna gani Sheria hii italinda ushahidi wenyewe? Je mtuhumiwa akiwa yuko nje hataweza kutumia njia mbalimbali kama rushwa au vitisho kwa mlalamikaji ili mwisho wa siku ushahidi kuharibiwa?

Ni kweli kwamba mtuhumiwa na mlalamikaji kila mmoja anatakiwa kupata haki anayostahili, mtuhumiwa hapaswi kuwekwa ndani bila upelelezi kukamilika, lakini pia mtuhumiwa kukaa nje wakati upelelezi unaendelea kunaweza kumnyima haki mlalamikaji ikiwa ni pamoja na kuhatarisha maisha yake. Nadhani suala la kumweka mtu ndani lengo lake kubwa ni kulinda ushahidi na kuwafanya mashuhuda washiriki kwa uhuru kuwezesha upelelezi kukamilika.

Natambua kuwa mapendekezo ya muswada huu yanahusu hasa makosa madogo, lakini inategemea kosa dogo ni kwa nani? Linaweza kuonekana kosa dogo lakini athari zake kwa mlalamikaji zikawa ni kubwa. Mfano, mtu anaweza kutuhumiwa kuiba kuku kwa macho ya kawaida ni kosa dogo ambalo upelelezi wake utafanyika mtuhumiwa akiwa nje, kumbe mwenye kuku alikuwa na mgonjwa hospitalini na kama angeuza kuku yule angelipata fedha ya dawa na kwa kukosa fedha hiyo mgonjwa anafariki kwa kukosa matibabu, tayari huyu mwizi wa kuku ametenda jinai “in direct”. Mheshimiwa Spika, kwa sababu na mimi naunga mkono mabadiliko haya ya sheria, ninayo mapendekezo. Moja, ni muhimu sheria itamke kipindi cha upelelezi namaanisha upelelezi uchukue muda gani kukamilika, pengine inaweza kuwa ngumu kutokana na aina ya makosa, lakini angalau inaweza kutamkwa kwa makosa haya na yale muda wake usizidi hapa, mbona faini na vifungo vimeainishwa kwa kila kosa, kwa nini iwe ngumu kwenye kuainisha muda wa uchunguzi kwa sababu hilo ndilo tatizo kwa mtazamo wangu. Nayasema haya kwa sababu hata sheria ikitungwa kwamba mtuhumiwa hatawekwa ndani au hatoshtakiwa mpaka upelelezi ukamilike kama tatizo liko kwenye upelelezi, maana yake tatizo litakuwa palepale sheria itakuwa haijatatua chochote tena kama mtuhumiwa hatoshikwa ndo kabisaa na jambo hili linaweza kufanya watu wajichukulie Sheria mkononi maana mtu kuwekwa kizuizini kuna mfanya pia awe salama dhidi ya aliyowatendea makosa.

Pili, kwa sababu lengo la Sheria hii ni kutaka kupunguza msongamano wa mahabusu magereza wakati fulani yafanyike mazungumzo kati ya walalamikaji na watuhumiwa, kuna wakati mlalamikaji hataki kuendelea na kesi na pengine ameshamsamehe mtuhumiwa au wakati mwingine ametambua kwamba alimsingizia dhamira inamsuta, hivyo anatamani kufanya mazungumzo na mtuhumiwa wayamalize na atoke, kwanini watu wa namna hiyo wasipewe fursa ya kukutana mbele ya vyombo vya sheria na kuyamaliza? Nadhani pia Sheria nyingi tulizo nazo ni za kikoloni wakati fulani tutatue haya masuala ya kisheria kimazingira. Ya nini kuendelea kumtunza mahabusu ambaye aliyemshitaki hataki tena kesi? Busara inatumika anatoka mambo yanaisha. Mashauri mengine yakimalizwa nje ya mahakama tutakuwa tumeisaidia sana serikali kuhudumia watu wasiostahili.

Nakuhakikishia Mheshimiwa Spika kwamba leo hii mahakama ikitangaza na kuweka utaratibu wa kuwakutanisha washitakianaji hasa wale ambao wametenda makosa madogo madogo utashangaa. Baadhi ya mahabusu hazitakuwa na watu kuna mtu yuko magereza kwa sababu tu alitukana, kosa ambalo ni la kimaadili na linalostahili pengine viboko kadhaa na akaendelea na shughuli nyingine za kujenga nchi. Watu kama hao wapewe fursa ya kukutana na waliowashtaki chini ya utaratibu maalumu lakini naona Sheria ya kutoshtakiwa mpaka upelelezi ukamilike haitatatua tatizo kwa kasi ya upelelezi haitawekewa ukomo katika makosa karibu yote.

Mwisho, nikuombe uyapokee maoni yangu haya, yanaweza yasiwe mazuri sana kutokana na sababu mbalimbali lakini nia yangu ni njema, pamoja na kwamba nafahamu mwisho wa kuwasilisha maoni haya kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilikuwa Februari 5, mwaka huu, sikuwa najua ni baada ya kufuatilia mjadala wa bunge. Lakini kwa sababu naona jambo hili lina maslahi mapana kwa nchi na wananchi kwa ujumla, nimeona nisinyamaze.

magabilomjalifu@gmail.com
ARUSHA-TANZANIA

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mitindo ya ‘ogelea piga mbizi’, Maquiz, ‘Chunusi,’ OSS ilivyotikisa mashabiki



Na Adam Fungamwango

MOJA ya miaka ya kufurahisha kwenye muziki wa dansi ni ile ambayo Maquiz Original walipoasisi mtindo wa ‘Ogelea piga mbizi’. Ilikuwa ni mwaka 1982. Ni baada ya kutoka kwenye mitindo mbalimbali kama vile ‘Chakula chakula kambombe’, ‘Kamanyola bila jasho’, na kwa muda mfupi ‘Scania LBT’.

Baada ya mitindo hiyo, Maquiz ambayo awali ilikuwa inaitwa Maquiz Du Zaire, licha ya kubadilisha majina ya mtindo, ilibadilisha na jina hilo, ikawa Maquiz Original.

Kwa mujibu wa kiongozi wa zamani wa bendi hiyo, Nguza Mbangu Viking, ni kwamba waliondoa maneno ya ‘du Zaire’ kutokana na kwamba wakati huo bendi haikuwa na wanamuziki Wazaire tu kama awali, bali walianza kuingia hata wanamuziki wa Kitanzania na mataifa mengine hadi raia wa Comoro.

Wakati Juwata Jazz Band na mtindo wao wa Msondo Ngoma wakiwa na upinzani mkali na DDC Mlimani Park Orchestra wana Sikinde Ngoma ya Ukae, kwa bendi za Kizaire wakati huo, sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kulikuwa na upinzani mkali kati ya Maquiz na Orchestra Safari Sound.

Na upinzani rasmi ulianza pale, Kikumbi Mwanza Mpango, King Kiki alipolipa kisogo kundi la Maqiuz du Zaire chini ya mtindo wa ‘Kamanyola bila jasho’, mwishoni kabisa mwa miaka ya 1990, na kujiunga na Orchestra Safari Sound. Ikumbukwe Kiki, alijiunga na Maquiz mwaka 1977, alipokwenda kuchulikuwa nchini Zaire baada ya kuonekana kuwa bendi ilihitaji mabadiliko.

Hakuwa mgeni nchini, kwani mwanzoni mwa miaka ya 1970 alikuwa hapa na bendi ya Orchestra Fauvette iliyotoka Zaire na kuingia nchini miaka hiyo. Kiki alikuwa mwimbaji na Freddie Ndala Kasheba alikuwa ni mpiga gita la solo wa bendi hiyo, wakatoa vibao vilivyopendwa mno si na Watanzania tu, bali Afrika Mashariki na Kati nzima kama ‘Jaqueline’, ‘Fransisca’, ‘Vivi’, ‘Nono na Kalimie’, ‘Zula’ na vingine vingi.

Bendi hiyo baada ya kurejea nchini Zaire, wanamuziki hao walikutana na wenzao na bendi ya Maquiz huko Lubumbashi, Kiki aliwaibia siri kuwa kuna soko kubwa la muziki nchini Tanzania. Ndipo Maquiz Du Zaire ilipofanya safari nchini Tanzania na kuweka makazi. Ilipoona upinzani wa muziki umekuwa mkubwa, ndipo walipomkumbuka mtu aliyewapa siri ya soko la muziki Tanzania, Kiki, wakamleta nchini mwaka huo.

Kwa kiasi kikubwa alibadilisha mno bendi hiyo na kubuni mtindo wa ‘Kamanyola bila jasho’. Ni kipindi ambacho si jina la Kiki tu kujulikana mpaka akapachikwa jina la King, lakini bendi ya Maquiz du Zaire ikapata mashabiki wengi na kuwa kivutio kikubwa. Ikarekodi nyimbo nyingi zilizopendwa kama ‘Kasongo’, ‘Nasema Sina Ndugu’, ‘Maggie’, ‘Dora Mtoto wa Dodoma’, ‘Chrismass’ na nyingine nyingi.

Mfanyabiashara matata wakati huo, Huggo Kisima, alimchomoa Kiki Maquiz du Zaire na kumpeleka kwenye bendi yake ndogo iliyoitwa Orchestra Safari Sound. Aliondoka pamoja na wanamuziki kadhaa. Huko akabuni mtindo wa ‘Masantula Ngoma ya Mpwita’. Ikawa balaa. Nyimbo za ‘Ni kweli’, ‘Mwaka wa Watoto’, ‘Haruna Kaka’, ‘Hangaika’, na zingine zilizifanya bendi hiyo kubwa kubwa. Na hapo ndiyo rasmi ilipoingia ushindani na Maquiz.

Hata hivyo, Kiki alimaliza mkataba wake miaka michache tu baadaye na kijiti kikachulikuwa na mwenzake aliyekuwa naye Fauvette, Ndala Kasheba. Wengi hawajui kuwa Kiki na Kaseba waliingia wote OSS ya Masantula, lakini hakukaa, kabla bendi haujarekodi akaelekea nchini Burundi. Mkataba wa Kiki ulipokwisha, Kisima alimleta Kesheba, ambaye yeye kwanza kabisa alikuja na gitaa la nyuzi 12. Kwa wakaida gitaa lina nyuzi sita, lakini yeye akaja na la nyuzi 12. Ikawa ni habari mpya nchini, mashabiki wakalipachika jina la ‘kombora’wengine wakaliita ‘dazani’.

Nyimbo za kwanza kabisa zilikuwa ni ‘Bakambi Nkela’, ‘Ashura’, ‘Maudhi ya Roho’, ‘Ntale’, ‘Mpakamanga’, ‘Marashi ya Pemba’, ‘Njiba’ na nyingine ambazo ziliitetemesha Maquiz Original ambayo tayari ilikuwa imemrudisha Kiki kundini, safari hii ikitoa nyimbo kama ‘Double Double’, ‘Anjelu’ ‘Mapenzi ya mashahidi’ na zingine, lakini hakukaa sana akaanzisha bendi ya Orchestra King Kiki Double O.

Ndipo Maquiz walipokuja na mtindo ya ‘Ogelea Piga Mbizi’.

Kuona hivyo Kasheba akaja na mtindo wa ‘Chunusi’, kwenye andishi lao kwenye matangazo magazetini waliandika kabisa kuwa usicheze na bahari kuna chunusi.

Yaani wote wanaoogelea, watakutana na chunusi. Yeye akajiita ndiyo chunusi mwenyewe. Ikawa inachorwa katuni kwenye magazeti jitu refu lililovaa kofia aina ya pama ambalo lipo katikati ya bahari, maji yamemfika kwenye magoti, akiangalia kama kuna mtu baharini. Hili lilileta upinzani mkubwa wa kimuziki baina yao. Ilisababisha kunyang’anyana mashabiki, na kukawa na upinzani wa maneno kati ya mashabiki wa pande zote mbili kama ule ubishani tunaouona wa Simba na Yanga mitaani.

Baadaye Maquiz wakapata wazo wakaja na neno ‘kafara’. Yaani humo kwenye bahari wamefanya kafara, hivyo wanaweza kuendelea kuogelea na kupiga mbizi.

Hata hivyo, wakaona isiwe tabu, wakaachana na mtindo huo, wakaja na ‘Sanifu’, baadaye ‘Zambwela’ hadi ‘Sendema,’. Mwaka 1985, Kasheba naye alimaliza mkataba wake, bendi ikawa chini ya Muhidini Gurumo na mtindo wa ‘Ndekule’, hapo ndipo upinzani rasmi wa OSS na Maquiz ulipokufa. Kwa sababu hakupiga muziki unaofanana kama mwanzo.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yoyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi.

# Mwisho wa Mauaji-1

Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

UMEITAZAMA vizuri hiyo picha?"

"Ndiyo baba."

"Hiyo ni picha ya mtu mmoja anaitwa Sabri Matata. Huyu mzee ana duka la nguo pale Ilala Bungoni." Sauti ya mzee Pokwa ilisikika vizuri. Japo alikuwa akiongea kivivuvivu na kwa utulivu, lakini alionekana kuwa makini.

Alikuwa amekaa kochi moja na kijana wake Prince.

"Huyu ikifika kesho saa nne usiku awe mgeni kule ahera. Nimekwambia saa hiyo kwa sababu duka lake anafunga saa tatu na nusu. Kumbuka ana gari huyu, kwa hiyo akitoka hapo huwa anakuja kuchukuliwa na kijana wake pale, au mkewe, ambao ndiyo huwa wanaendesha. Sasa mpaka afunge, atie makomeo yake, apande kwenye gari, nadhani itakuwa ni saa nne. Kwako ni kazi ndogo sana. Ni kufyatua kitufe tu, halafu risasi ndiyo inafanya kazi ya kwenda kwenye mwili wake, biashara inakwisha. Kwa wewe sina shaka hata kidogo. wakati anafungua mlango wa gari, nataka risasi iwe tayari imepenya kichwani kwake."

Prince alimtazama vizuri baba yake. Alimuelewa vizuri. Hata hivyo alikuwa hajawahi kuua mtu hata siku moja.

Ambacho anachofahamu, ni kwamba wakati anapata akili tu, baba yake alikuwa akimchukua na kwenda naye kwenye moja ya mapori ya mkoa wa Pwani na kufanya naye mazoezi ya kulenga shabaha.

Tangu mdogo ilikuwa ndiyo kazi yake. Anakumbuka kila Jumamosi na Jumapili, kazi ilikuwa ndiyo hiyo. Awali ilikuwa ngumu, lakini kadri muda ulivyozidi alianza si tu kuizoea, bali kuipenda pia. Kwake ilianza kuwa kama mchezo wa kitoto.

Wakati watoto wenzake wakichezea vigari, na matoi mengine ya kitoto, yeye alifundishwa jinsi ya kulenga shabaha. Mzee Pokwa alikuwa mtaalam mno wa kulenga shabaha. Alimfundisha Prince akaiva.

Lakini alikuwa akijiuliza siku zote, ni kwa nini anafundishwa yote haya? Kwa nini baba yake amekuwa akitilia mkazo suala hili kuliko hata masomo ya kawaida?

Wakati akiona watoto wenzake wakienda shule, yeye aliletewa walimu nyumbani hapo. Na hii ni baadaye ya yeye mwenyewe kumuuliza baba yake juu ya kumpatia elimu.

Na kweli alisoma na kuelimika kwa kiasi kikubwa, ingawa hakwenda shule yoyote ile.

Kwa mara ya kwanza alihisi kuwa huenda kile ambacho baba yake alikuwa akimfundisha miaka yote ile akiwa bado mdogo ndiyo hiki kinaanza kutimia.

"Sawa baba, lakini kwa nini huyu mzee afe?"

Kilifuatia kicheko kikali kutoka kwa mzee Pokwa.

"Najua wewe ndo kijana mdogo, lakini sikujua kuwa kumbe bado mdogo kihivyo. Hakuna mtu ambaye anaua bila sababu. Kuua mtu ni jambo la mwisho kabisa kwa uamuzi wa binadamu. Ukiona nimesema hivyo, ujue ni jambo kubwa. Hivi umeshawahi kuniona nakuja na mwanamke hapa?"




**Tangu mdogo ilikuwa ndiyo kazi yake. Anakumbuka kila Jumamosi na Jumapili, kazi ilikuwa ndiyo hiyo. Awali ilikuwa ngumu, lakini kadri muda ulivyozidi alianza si tu kuizoea, bali kuipenda pia. Kwake ilianza kuwa kama mchezo wa kitoto.**

"Hapana baba, sijawahi kukuona."

"Mwanangu Prince, umeshawahi kuona, au kusikia habari yoyote kuwa una mdogo wako, dada yako, kaka yako, au ndugu yako wa damu?"

"Hapana baba, sijawahi."

"Basi ndiyo ujue kuwa dunia hii ni mbaya. Dunia ni tambara bovu. Usimuamini mtu yoyote katika dunia hii. Na kila siku nimekuwa nikikufundisha hili muda wote wakati ukikua, si ndiyo?"

"Ndiyo baba, lakini zamani ulikuwa unaniambia, lakini mimi niliona kama maneno tu ya baba anamwambia mtoto wake, sijaona, au kujua umuhimu wa maneno haya. Yanahusiana nini na hili?"

Maneno ya mzee Pokwa yalimshtua kijana wake. Ni kweli amekuwa akiishi maisha ya upweke mno. Imefikia wakati ameyazoea, kiasi kwamba ameyaona ya kawaida tu. Wala hakuwa na haja ya kuanza kumuuliza baba yake kama ana ndugu au hana. Anakumbuka kuwa wakati akiwa mdogo, alimuuliza baba yake swali hilo na kujibiwa.

"Ukikua nitakwambia, kwa sasa hata nikikwambia hutoelewa, wewe bado mtoto mdogo, hutakiwi kuambiwa mambo makubwa, soma, fanya mazoezi, cheza, kula, kunywa na pumzika."

Tayari Prince alikuwa ameshaiangalia vya kutosha picha ile, na akaiweka mezani, ambapo pia kulikuwa na bastola. Ni bastola ambayo kila anapokwenda iko kibindoni.


"Mwanangu kwenye dunia hii, adui yako ni yule unayekula naye. Hakuna mtu yoyote anayeweza kukudhuru ambaye hakujui. Ataanzia wapi? Asiyekujua hawezi kuwa karibu na wewe. Ili mtu akudhuru, jambo la kwanza ni lazima awe karibu na wewe. Ndiyo maana siku zote nakwambia, usiwe sana na ukaribu na watu. Mtu anaanza kwanza kuwa karibu na wewe, halafu ukishamuamini, ndipo anatumia fursa hiyo kukudhuru. Wale waliosema kikulacho ki nguoni mwako hawajakosea. Kunguni wanaokung'ata wako kitandani mwako, hawawezi kufanya hivyo kama wapo kwenye kitanda cha mtu mwingine." Pokwa aliendelea na tabia yake ya kumjaza falsafa zake kijana wake Prince. Naye alikuwa ameshashiba, kuzizoea na kuziishi.

"Maisha yote unayoishi, ingawa unaishi kwenye nyumba nzuri, unapata kila kitu, baba yako nina mali nyingi, lakini upweke huu tulionao mimi na wewe, unasababishwa na watu kama hawa. Unasababishwa na mzee Sabri na wenzake. Mwanangu nenda kwanza kammalize. Ukifanikiwa nitajua sasa umekuwa. Umekuwa mkubwa, na hapo nitakueleza kila kitu."

Maneno yaliingia kwenye ubongo wa Prince. Hata hajui ndugu yoyote wa mama yake, hamjui mama yake. Hana kaka, dada wala ndugu wa damu. Kumbe ni kwa sababu ya Sabri? Damu ilianza kumchemka mwilini. Akapeleka mkono mezani na kuinua bastola yake. Akaitazama. Akaibusu.

"Nitakwenda baba, nina hamu sasa ya kutaka kujua juu ya familia yangu. Mama yangu, ndugu zangu na kila kitu kilichojificha ambacho unataka kuniambia."

ITAENDELEA JUMAPILI



# COUNTRY WEEZY ALALAMA KUNA MKONO WA MTU

RAPA mwenye msimamo mkali, Country Weezy, amesema kuna figisu ambazo anaona anafanyiwa na baadhi ya watu wasiomtakia mema.

Amesema watu hao wanataka kudukua akaunti yake ya Instagram na ile ya Youtube.

"Kwa muda wa wiki naona akaunti yangu ya Youtube kuna raia kwa hisia zao binafsi wanajaribu kudukua, kwanza nilifika wafuasi laki tatu, lakini walianza kupungua". ameandika

Akasisitiza "Kuna mkono wa mtu unaendelea, sio tu youtube mpaka instagram naona mkono wa mtu unavoendelea. Nasisitiza kama kijana nilijeajiri kupitia sanaa yangu," anasema.

# 'Nzela'ya Mr Lap kuitikisa Afrika Mashariki

**KINSHASA,** DRC

TASNIA ya muziki Afrika Mashariki inatarajia kushuhudia mapinduzi makubwa ya muziki kutokea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kupitia lebo ya Visionnaire Team.

Lebo hiyo kwa sasa inamsimamia msanii wa kizazi kipya Lwindi Pascal, maarufu kama Mr Lap ambaye wiki inayokuja anaachia albam yake mpya inayoitwa Nzela.

Akizungumza na gazeti hili, Mr Lap amesema yupo kwenye lebo ya Visionnaire Team tangu mwaka 2021, na Nzela ni albamu yake ya kwanza ikiwa na jumla ya nyimbo 10.

"Nzela ni lugha ya Lingala ina maanisha barabara au Njia na nimeiita hivyo kwa sababu hii ni albamu itakayonifungulia njia. Ndani kuna kolabo tatu nikiwashirikisha na wasanii wa Congo DRC," amesema Mr Lap.

Nyimbo zilizokuwemo katika albamu hiyo ni Forever Boulogue, Zambe ft Young BOB,No Body, Story, Tabiya, Come Close ft La Cleopatre Marina, Aziza, , Retard ft Too Kelly na Pata Makuta.

Ameongeza kusema "Baada ya kuachia albamu hii nitafanya ziara ya matamasha katika miji mbalimbali hapa Congo, Bujumbura, Kigoma, Dar Es Salaam, Kampala na sehemu zingine," amesema Mr Lap.

Aidha ameeleza mbali na kuachia albamu hiyo Mei 24, mwaka huu mashabiki wajiandae kwa video kali ya wimbo wake Tabia itakayokuwa kwenye chaneli yake ya YouTube.

Nyimbo zilizokuwa katika Albamu hiyo zina mchanganyiko wa muziki wa aina mbalimbali kama Rumba, Afrobeat, Amapiano na Afropop.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POGBA ATAKIWA**

MANCHESTER City wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, kwa uhamisho huru. ***(Mail)***

**POTTER KUMRITHI CONTE**

KOCHA wa Brighton, Graham Potter ndiye anayependelewa kuchukua nafasi ya Antonio Conte kule Tottenham Hotspur. Brighton watataka fidia ya pauni milioni 10 kutoka kwa Spurs iwapo Conte ataondoka mwishoni mwa msimu. ***(Telegraph)***

**HAG KUMBAKIZA RONALDO**

KOCHA ajaye wa Manchester United, Erik ten Hag anamtaka mshambuliaji, Cristiano Ronaldo kubakia katika klabu hiyo. Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa hapo Old Trafford. ***(Telegraph)***

**BREMER ATAKIWA CHELSEA**

CHELSEA wanaangalia uwezekano wa uhamisho kwa ajili ya mlinzi Mbrazili Gleison Bremer mwenye umri wa miaka 25. ***(Football London)***

**EKITIKE AWANIWA MAN**

MANCHESTER United pia wana nia ya kumchukua mshambuliaji Mfaransa wa klabu ya Reims, Hugo Ekitike mwenye umri wa miaka 19. ***(Mail)***

**CARVALHO WA LIVERPOOL**

KOCHA wa Fulham, Marco Silva amesema mshambuliaji, Fabio Carvalho anaweza kuuzwa wakati wa dirisha la majira ya joto. Liverpool wamekubali kutoa pauni milioni 7 ili kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(Liverpool Echo)***

**ERIKSEN KUBAKI**

NYOTA Christian Eriksen anaangalia uwezekano wa kubakia katika klabu ya Brentford msimu ujao. Kiungo huyo wa kati wa Denmark mwenye umri wa miaka 30, amekuwa akihusishwa na taarifa za kurejea tena katika Tottenham na kuhamia Leicester. ***(Telegraph)***

**MELO ATAKIWA ARSENAL**

Klabu ya Arsenal inamtaka kiungo wa kati wa Juventus, Mbrazili Arthur Melo mwenye umri wa miaka 25. ***(Ekrem Konur)***

**MBAPPE KUAMUA**

MSHAMBULIAJI Mfaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, atatangaza uamuzi wake wa mwisho juu ya iwapo ataondoka au kubaki Paris St-Germain, Juni. ***(Le Parisien)***


**BROWNHILL AWINDWA**

WEST Ham wanaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Bunley mwenye umri wa miaka 26, Brownhill. ***(90Min)***

**NYOTA KUONDOKA LEICESTER**

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers ameazimia kukibadilisha kikosi chake katika hatua inayoweza kupelekea wachezaji kadhaa kuondoka katika klabu hiyo. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA KUTUA CITY

### Mwenyewe abainisha kutaka kufanya kazi na Guardiola, huku mshahara wake...

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imekuwa muwindaji wa kushitukiza kwa kiungo wa kati wa Manchester United, Paul Pogba ambaye mkataba wake unakamilika mwishoni mwa msimu huu.

Pogba mwenye umri wa miaka 29 hapo awali alinukuliwa kuhusu kujutia uhamisho wake wa kwenda Old Trafford, na alitarajiwa kuondoka kwenye Ligi Kuu ya England katika dirisha lijalo la usajili, akihusishwa zaidi na Barcelona na Real Madrid.

Licha ya Mfaransa huyo kuweka wazi nia yake ya kutaka kutwaa mataji, huenda asilazimike kuondoka katika jiji hilo ili kupata matakwa yake, akiwa na nafasi ya kutua Man City ikiwa ataachana na Mashetani wekundu hao.

**Gazeti la Daily Mail limeripoti kuwa City wana nia ya kumnunua Pogba kwa uhamisho wa bure, wakati gazeti la Guardian limedai kiungo huyo wa kati wa Ufaransa angependa kufanya kazi na kocha Pep Guardiola, na kwamba klabu hiyo iko tayari kutoa mkataba wa miaka minne.**

Iwapo atachukua hatua hiyo, Pogba atakuwa ndio jina kubwa zaidi kuwahi kuhama Man United na kwenda Man City baada ya Carlos Tevez.

Lakini ripoti ya gazeti la Guardian limebainisha kuwa atalazimika kupunguza mshahara wake ili kutua huko.

Haijulikani ikiwa ofa kutoka Hispania zitakuwa na faida kubwa kifedha, lakini hakuna timu inayoweza kutoa nafasi nzuri zaidi ya mafanikio ya Ulaya zaidi ya Man City.

Katika mechi 154 za Ligi Kuu tangu alipowasili mwaka 2016, Pogba amefunga mabao 29 na kutoa pasi za mabao 41.

SportPesa LIVE IN PLAY

MECHI KALI
ATLETICO MADRID
VERSUS
REAL MADRID
1 | 2.06
X | 3.45
2 | 3.40

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BAYERN YAKOMAA KUMBAKISHA LEWANDOWSKI

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA Julian Nagelsmann amesema Bayern Munich wamefanya mazungumzo ya kutia moyo kuhusu mkataba mpya na wakala wa Robert Lewandowski huku kukiwa na taarifa za kutakiwaa Barcelona.

Lewandowski mkataba wake wa sasa na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, unakamilika Juni 2023 na Barca wanahusishwa na kutaka kumnunua mshambuliaji huyo.


Uongozi wa Bayern umekutana na Pini Zahavi, wakala wa Lewandowski, huku miamba hao wa Bavaria wakijaribu kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33. Nagelsmann ana matumaini kwamba makubaliano yanaweza kufikiwa.

Nagelsmann alisema: "Niliuliza ikiwa yalikuwa mazungumzo mazuri. Na inaonekana kwamba ilikuwa hivyo. Lakini hakuna cha kuzungumza kwa sasa.

"Msimamo wangu haujabadilika, tunataka kuuweka kama ulivyo na kuongeza mkataba wake."

Nagelsmann yuko tayari kumsubiri Lewandowski kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake. Aliongeza: "Unajua kwamba Pini anapenda kujadiliana na hivyo unahitaji subira kidogo."

Lewandowski wiki iliyopita amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga angalau mabao 34 kwenye Bundesliga katika misimu mitatu mfululizo.



# Chelsea yauzwa rasmi

**LONDON,** England

CHELSEA wameingia makubaliano ya kuuzwa kwa klabu hiyo kwa kundi la umiliki linaloongozwa na Todd Boehly, Clearlake Capital, Mark Walter na Hansjoorg Wyss kwa pauni bilioni 4.25.

Muungano huo unaoongozwa na Boehly ulikuwa umejiweka wazi katika kinyang'anyiro cha kuwanunua The Blues hao baada ya kuchaguliwa kama mzabuni aliyependekezwa licha ya ofa ya mwisho kutoka kwa bilionea wa Uingereza, Jim Ratcliffe.

Baada ya kuuzwa kwa klabu hiyo, sasa wamiliki hao wapya wanatakiwa kuweka pauni bilioni 1.75, mpango unaotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Katika taarifa iliyotolewa alfajiri ya jana Jumamosi na klabu ya Chelsea ilisema: "Kati ya uwekezaji wote unaofanywa, pauni bilioni 2.5 zitatumika kununua hisa za klabu na mapato hayo yatawekwa kwenye akaunti ya benki ya Uingereza iliyofungiwa kwa nia ya kuchangia asilimia 100 kwa misaada ya kwenda nchini Ukraine kwa waathirika wa vita kama ilivyothibitishwa na Roman Abramovich.

CHEZA USHINDE KASINO




# WAKENYA, WATANZANIA WAGAWANA DHAHABU

**Mwandishi Wetu,** MBEYA

WANARIADHA Watanzania wamegawana medali za dhahabu na wale Wakenya katika mbio za Mbeya Tulia Marathoni (MTM) iliyofikia tamati jana kwenye uwanja wa Sokoine jijini hapa, zilizoandaliwa na Taasisi ya Tulia Trust.

**Watanzania, Emmanuel Giniki na Marcelina Mbua walitwaa medali hizo kwenye mbio za kilomita 21 (nusu marathoni) wakati kwenye marathoni (kilomita 42) Wakenya, Erick Kiptoo na Daisy Kipsligati walitwaa ubingwa.**

Giniki ametwaa ubingwa kwa wanaume kwenye mbio za kilomita 21 akikimbia kwa saa 1:03:52 huku Marcelina akitwaa ubingwa kwa wanawake akitumia saa 1:12:32

Kiptoo alikimbia na kumaliza kilomita 42 kwa saa 2:17:53 kwenye mbio ndefu za barabarani zilizoongozwa na Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson ambaye alizizindua akiwa na baadhi ya viongozi wengine wakiwamo wa wizara ya michezo, wabunge na wanariadha nyota wa zamani wakiongozwa na washindi wa Olimpiki, Filbert Bayi na Suleiman Nyambui.

Ikipewa mzuka na wadhamini mbalimbali ikiwamo benki ya CRDB, ORYX gesi, Mbeya Cement na Mamlaka ya Bandari (TPA), Dk Tulia alikimbia na kumaliza kilomita 5, kabla ya kuwavalisha medali mabingwa na wakimbiaji mbalimbali waliokimbia na kumaliza mbio.

Kwenye kilomita 21, nafasi ya pili ilichukuliwa na Joseph Panga aliyekimbia kwa saa 1:04:15 na Kipruto wa Kenya alihitimisha tatu bora akitumia saa 1:06:15 huku bingwa wa zamani wa dunia, Fabiano Joseph akimaliza wa nane.

Kwa wanawake, Marcelina Mbua alimaliza kinara akifuatiwa na Magdalena Shauri aliyekimbia kwa saa 1:14:13 na Jackline Sakilu alihitimisha tatu bora kwa saa 1:15:22 na Failuna saa 1:15:52.

Kwenye marathoni, nafasi ya pili ilichukuliwa na Abraham Too na Rosina Kiboino wote kutoka Kenya huku Sarah Ramadhan na Emmanuel Gadiye wa Tanzania wakihitimisha tatu bora kwa wanaume na wanawake.

Akifunga mbio za msimu huu, Spika wa Bunge, Tulia alisema zimekuwa chachu ya wanariadha kujitokeza kwa wingi kushiriki.

"Mbeya Tulia Marathoni imekuwa ikipiga hatua kila mwaka, msimu huu hamasa imekuwa kubwa na tunaamini inakwenda kuleta mabadilliko makubwa kwenye riadha yetu hasa kwa wanariadha wa mbio za uwanjani na wale wa marathoni," alisema.

Aliongeza lengo la mbio hizo ni kukusanya fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu na afya kwenye jiji la Mbeya, lakini pia kwenye mikoa mingine huku akiwashukuru wadhamini wote ambao wameshiriki kufanikisha mbio za msimu huu.



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson akimpongeza bingwa wa tano wa mbio za Mbeya Tulia Marathoni, Daisy Kipsliguti kutoka Kenya baada ya kuibuka mshindi hapo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dullah Mbabe aibuka mbabe

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Abdallah Pazi 'Dullah Mbabe' amemchapa mpinzani wake Ramadhan Migwede kwa KO ya raundi ya saba katika pambano maalum la kimaonyesho 'Exibition fight' lililofanyika juzi usiku kwenye Ukumbi wa Iwawa uliopo Masasi.

Pambano hilo lilikuwa maalum kwa ajili ya kuhamasisha mchezo wa ngumi za kulipwa kuelekea katika pambano la 'Payback Night' usiku wa deni litakalowakutanisha bondia wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania 'JWTZ', Seleman Kidunda dhidi ya Tshimanga Katompa, litakalofanyika Julai 30, mwaka huu, Uwanja wa Majimaji Songea, Mkoani Ruvuma.

Katika pambano hilo ambalo lilikuwa la raundi nane, Dullah alifanikiwa kushinda kwa KO katika raundi saba baada kumchapa gumi kali mpinzani wake na kuepelekea kushindwa kuendelea na mwamuzi, Mwinyi Mila alimaliza baada ya kumhuhesabia hadi kumi.

Akizungumza mara baada ya kushinda pambano, Dullah aliwashukuru wadau na mashabiki waliojitokeza kwenye pambano hilo ambalo anaamini litaleta chachu ya maendeleo katika mchezo huo akiwataka viongozi kujitoa katika kuusaidia.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAPILI - 08/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 4798 | NEC Nijmegen vs GO Ahead Eagles | 2.10 | 3.31 | 3.31 |
| 13:30 | 5011 | Spezia vs Atalanta | 5.75 | 4.66 | 1.45 |
| 14:00 | 1104 | Ufa vs Rostov | 2.35 | 3.16 | 2.96 |
| 14:00 | 2108 | Metz vs Lyon | 6.57 | 4.88 | 1.39 |
| 15:00 | 2506 | Getafe vs Rayo Vallecano | 2.05 | 3.00 | 4.00 |
| 15:30 | 1098 | Vitesse Arnhem vs Heerenveen | 1.82 | 3.62 | 3.92 |
| 15:30 | 2740 | AZ Alkmaar vs Ajax | 4.34 | 3.90 | 1.69 |
| 16:00 | 1376 | Reims vs Lens | 3.24 | 3.29 | 2.16 |
| 16:00 | 1930 | Venezia vs Bologna | 2.87 | 3.36 | 2.30 |
| 16:00 | 2408 | Arsenal vs Leeds | 1.49 | 4.31 | 5.62 |
| 16:00 | 2412 | Clermont Foot vs Montpellier | 1.86 | 3.69 | 3.74 |
| 16:00 | 2703 | Leicester vs Everton | 2.53 | 3.22 | 2.68 |
| 16:00 | 2782 | Angers vs Bordeaux | 2.12 | 3.34 | 3.29 |
| 16:00 | 3647 | Yeni Malatyaspor vs Caykur Rizespor | 3.68 | 3.63 | 1.90 |
| 16:00 | 5043 | Altay vs Giresunspor | 2.36 | 3.34 | 2.84 |
| 16:00 | 5357 | Norwich City vs West Ham | 4.25 | 3.66 | 1.75 |
| 16:30 | 2522 | Arsenal Tula vs FC Krasnodar | 2.77 | 3.46 | 2.32 |
| 16:30 | 3983 | Eintracht Frankfurt vs Monchengladbach | 2.26 | 3.78 | 2.69 |
| 17:00 | 4943 | Rangers vs Dundee Utd | 1.16 | 6.76 | 14.91 |
| 17:00 | 5118 | Viktoria Plzen vs Sparta Prague | 1.97 | 3.58 | 3.68 |
| 17:15 | 3878 | Villarreal vs Sevilla FC | 2.29 | 3.26 | 3.06 |
| 17:30 | 1275 | Lausanne-Sport vs FC Basel | 3.84 | 3.79 | 1.82 |
| 17:30 | 1693 | FC Luzern vs Servette Geneva | 2.58 | 3.42 | 2.53 |
| 17:30 | 4817 | FC Vizela vs Maritimo | 2.07 | 3.32 | 3.42 |
| 17:45 | 2674 | Feyenoord vs PSV Eindhoven | 2.33 | 3.59 | 2.69 |
| 18:00 | 2513 | Austria Vienna vs Rapid Vienna | 2.10 | 3.41 | 3.02 |
| 18:00 | 2884 | PAS Giannina vs PAOK | 4.08 | 3.13 | 1.96 |
| 18:05 | 2500 | Lorient vs Marseille | 3.85 | 3.65 | 1.85 |
| 18:30 | 1447 | Kaizer Chiefs vs Mamelodi Sundowns | 3.92 | 2.93 | 2.07 |
| 18:30 | 2436 | Bayern Munchen vs Stuttgart | 1.22 | 6.50 | 9.26 |
| 18:30 | 2762 | Kalmar vs Hammarby | 3.26 | 3.31 | 2.04 |
| 18:30 | 4654 | Manchester City vs Newcastle | 1.19 | 6.13 | 13.13 |
| 19:00 | 1655 | Stromsgodset vs Rosenborg | 2.63 | 3.33 | 2.53 |
| 19:00 | 2594 | Besiktas vs Fenerbahce | 2.50 | 3.45 | 2.60 |
| 19:00 | 3134 | Salernitana vs Cagliari | 2.32 | 3.27 | 2.92 |
| 19:00 | 3697 | Haugesund vs Kristiansund | 2.09 | 3.38 | 3.33 |
| 19:00 | 4068 | Lokomotiv Moscow vs Rubin Kazan | 1.90 | 3.56 | 3.66 |
| 19:00 | 5280 | Bodo Glimt vs Lillestrom | 1.55 | 4.31 | 5.01 |
| 19:00 | 5515 | Aalborg vs Midtjylland | 2.99 | 3.49 | 2.20 |
| 19:30 | 2166 | Espanyol vs Osasuna | 2.32 | 3.21 | 3.06 |
| 19:30 | 3262 | Royal Antwerp vs Anderlecht | 3.23 | 3.47 | 2.09 |
| 20:00 | 3976 | Sporting Braga vs FC Arouca | 1.65 | 3.74 | 4.99 |
| 20:30 | 1206 | RB Leipzig vs Augsburg | 1.23 | 5.96 | 9.94 |
| 21:00 | 2185 | Aarhus vs Sonderjyske | 1.91 | 3.53 | 3.73 |
| 21:00 | 5064 | Ham-Kam vs Aalesunds | 2.03 | 3.34 | 3.53 |
| 21:45 | 1504 | Paris St Germain vs Troyes | 1.20 | 6.27 | 12.20 |
| 21:45 | 2742 | Verona vs AC Milan | 4.26 | 3.82 | 1.71 |
| 22:00 | 4906 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.06 | 3.45 | 3.40 |
| 22:30 | 1111 | Santa Clara vs Pacos Ferreira | 2.07 | 3.33 | 3.43 |
| 23:00 | 4124 | Vancouver Whitecaps vs Toronto FC | 1.94 | 3.73 | 3.63 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Mei 8, 2022

Nipashe




Pogba kutua Man City UKURASA 21



Walinzi wa Simba, Pascal Wawa (kushoto) na Erasto Nyoni wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara dhidi ya Ruvu Shooting utakaopigwa leo Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

## Yanga kuivaa Prisons bila majeruhi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema kuwa itaingia kwenye mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara siku ya Jumatatu dhidi ya Prisons bila ya kuwa na majeruhi yoyote yule.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli amesema kuwa hata Yacoub Songne ambaye ndiye majeruhi wa muda mrefu amepona kabisa, ila bado hajaruhusiwa kucheza kwa sababu madaktari bado wameona aendelee kwanza kuwa chini ya ungalizi wao.

"Kikosi kilirejea salama kutoka Kigoma na kimeingia kambini Ijumaa kujiwinda na Prisons siku ya Jumatatu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. Tunachoshukuru ni kwamba tulikwenda Kigoma na wachezaji 22 na tumerudi nao wakiwa wazima wa afya, hatukupata majeruhi kwenye mchezo wetu dhidi ya Ruvu Shooting Jumatano iliyopita, wala kwenye mazoezi. Kwa sasa hatuna majeruhi yoyote yule kati ya wachezaji wetu wote 30, hata Yacouba ameshapona, ila madaktari wameona bado aendelee kwanza kuwa chini ya uangalizi kwa muda mfupi wajiridhishe kabla ya kumruhusu kucheza," alisema Bumbuli.

Kuhusu suluhu dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, aliwaomba radhi wanachama na mashabiki wa timu hiyo mkoani humo kwa kutopata ushindi, lakini akawashukuru kwa mapokezi makubwa, ingawa hawakuwapa kile kilichostahili.

# Simba pointi 3 muhimu leo

## ● ● ● Yaivaa Ruvu Shooting ambayo inapambana kubaki Ligi Kuu na kumaliza uteja, huku...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

SIMBA inashuka dimbani leo kusaka pointi tatu dhidi ya Ruvu Shooting mchezo wa Ligi Kuu Tanzania, utakaopigwa katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Wekundu wa Msimbazi hao watamkosa kiungo mkabaji wao Sadio Kanoute aliyepewa mapumziko ya wiki mbili baada ya kuumia kwenye mchezo dhidi ya Yanga.**

Kanoute aligongana na mguu na kiungo wa Yanga, Khalid Aucho na kushindwa kuendelea na mchezo na kudhaniwa amepata madhara makubwa, lakini baada ya vipimo vya madaktari ameonekana hana tatizo.

Nyota huyo anatarajia kurudi uwanjani Mei 22, mwaka huu katika mchezo wa ligi hiyo dhidi ya Geita Gold FC, uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Kuelekea mchezo huo, timu zote hizo zinashuka dimbani zikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare. Simba ikitoka sare dhidi ya Namungo FC, uwanja wa Ilulu, Lindi. Ruvu ikitoka suluhu na Yanga katika uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola alisema maandalizi yanaendelea vizuri na wamejipanga kutafuta pointi tatu katika mchezo huo.

Alisema watawakosa baadhi ya wachezaji ambao ni majeruhi akiwemo Kanoute, mbali na huyo wote wako vizuri na tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya.

"Hatukuwa na matokeo mazuri katika michezo yetu mitatu, benchi la ufundi tulikaa na kukubaliana kuhusu mwenendo wa timu katika mechi hizo na tumerejea kwa wachezaji na kuweka mipango ya mechi ijayo dhidi ya Ruvu Shooting tupate ushindi," alisema Matola.

Alisema wanaenda kupambana na kutafuta matokeo mazuri kwa sababu ya kupunguza presha ya uwiano wa pointi na Yanga inayoongoza msimamo wa Ligi.

"Kiufundi mchezo utakuwa mgumu kwa sababu ya wapinzani wetu nao hawako katika nafasi nzuri katika msimamo, tunaingia kwa tahadhari kubwa kwenda kutafuta pointi tatu muhimu," alisema Matola.

Naye Kocha Msaidizi wa Ruvu, Mohammed Nakuchema alisema wamejipanga vizuri kwenda kutafuta matokeo dhidi ya Simba na kufuta uteja kwa wapinzani wao hao.

"Tumejipanga kutafuta matokeo muhimu katika mchezo huo, Simba ni timu nzuri, na hivyo tunaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa.

Alisema hawatakuwa na mabadiliko yoyote katika kikosi kitakachoshuka dimbani leo dhidi ya Simba na kile kilichocheza hivi karibuni dhidi ya Yanga.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >